# TANZANIA

## RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA MWAKA 2019

### MUHTASARI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni jamhuri ya vyama vingi vya siasa inayojumuisha bara na visiwa vya Zanzibar vyenye utawala kiasi, ambapo visiwa vyake vikuu ni Unguja (Kisiwa cha Zanzibar) na Pemba. Muungano huo unaongozwa na rais, ambaye pia ni mkuu wa serikali. Chombo chake chenye muundo wa baraza moja la kutunga sheria ni Baraza la Kitaifa (bunge). Ingawa Zanzibar ni sehemu ya muungano, inatumia uhuru mkubwa na ina serikali yake pamoja na rais, mfumo wa mahakama, na baraza la kutunga sheria, na kwa kiasi kikubwa inajitawala. Mwaka 2015 nchi hiyo ilifanya uchaguzi wake mkuu wa tano wa vyama vingi. Upigaji kura katika uchaguzi wa muungano na Zanzibar kwa kiasi kikubwa ulionekana kuwa huru na wa haki, na hivyo kupelekea kuchaguliwa kwa rais wa muungano (John Magufuli). Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, hata hivyo, alitangaza kufutwa kwa uchaguzi sambamba wa rais na wa baraza la wawakilishi Zanzibar baada ya kiasi fulani tu cha kura kuhesabiwa, na hivyo kuibua mgogoro wa kisiasa visiwani. Uchaguzi mpya uliofanyika Zanzibar mwaka 2016 haukuwa jumuishi wala wakilishi, hususan tangu chama kikuu cha upinzani kilipoamua kutoshiriki; rais aliyekuwepo madarakani (Ali Mohamed Shein) alitangazwa kuwa mshindi kwa kupata asilimia 91 ya kura.

Chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ni ya muungano, Jeshi la Polisi la Tanzania (TPF) lina jukumu la msingi la kudumisha sheria na utulivu nchini. Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), kitengo maalum cha TPF, kina jukumu la msingi la kudhibiti maandamano haramu na ghasia. Jeshi la wananchi wa Tanzania linajumuisha Jeshi, Jeshi la Majini, Kamandi ya Anga na Jeshi la Kujenga Taifa. Wanawajibikia usalama wa nje lakini pia wana baadhi ya majukumu ya usalama wa ndani na wanaripoti Wizara ya Ulinzi. Mamlaka za kiraia zilidumisha udhibiti wenye ufanisi juu ya majeshi ya usalama na pia zilielekeza harakati zao.

Masuala muhimu ya haki za binadamu yalijumuisha: mateso, kuwekwa kizuizini kiholela; hali ngumu na za kutishia maisha gerezani; wafungwa wa kisiasa;

uingiliaji wa kiholela na haramu katika faragha ya mtu; aina mbaya sana za vizuizi juu ya uhuru wa kujieleza, vyombo vya habari, na intaneti; ukatili; vitisho vya ukatili, au ukamataji usio wa haki au mashtaka dhidi ya waandishi wa habari, udhibiti, na kuzuia tovuti; kuwepo kwa sheria ya kashfa ya uhalifu; kuingilia kwa kiasi kikubwa haki ya kukusanyika kwa amani na uhuru wa ushirikiano, kama vile sheria zinazozuia vikali mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO); kuwapeleka kwa nguvu wakimbizi katika nchi ambako wanaweza kukabiliwa na vitisho kwa maisha yao au uhuru wao kulingana na rangi yao, dini, uraia, uanachama katika kundi mahususi la kijamii, au maoni ya kisiasa, au kuwatesa wakimbizi ambako kunaweza kujumuisha ukiukaji wa haki za binadamu; vizuizi kwa ushiriki wa kisiasa pale serikali isipochaguliwa au uchaguzi umegunduliwa haukuwa wa kweli, huru, au haki; rushwa ilioenea; usafirishaji haramu wa binadamu; ukatili wa kihalifu dhidi ya wanawake na wasichana, ambapo serikali ilichukua hatua kidogo kuzuia au kushtaki; uhalifu unaohusisha ukatili au vitisho vya ghasia vinavyolenga watu wenye ulemavu, wanachama wa walio wachache kitaifa/kirangi/kimbari, au watu asilia; uhalifu unaohusisha ukatili au vitisho vya ukatili vinavyolenga wasagaji, mashoga, watu wanaofanya mapenzi na jinsia zote mbili mwanamke na mwanaume, watu waliozaliwa na jinsia ya kike au ya kiume wanaojihisi wako tofauti na jinsia waliyozaliwa nayo, au watu waliozaliwa wakiwa na umbo la kike au kiume lakini ndani wana sifa za jinsia tofauti na maumbile yao (LGBTI); kuwepo au matumizi ya sheria zinazoharamisha tabia ya watu wazima kukubaliana kufanya mapenzi ya jinsia moja; matumizi ya nguvu au kulazimisha ajira kwa watoto, kama ilivyoorodheshwa katika ripoti ya Wizara ya Kazi kuhusu Aina Mbaya Sana za Ajira kwa Watoto.

Katika visa vingine serikali ilichukua hatua za kuchunguza na kushtaki maafisa waliofanya dhuluma za haki za binadamu, lakini kuepuka adhabu kwa polisi na vikosi vingine vya usalama na matawi ya kiraia ya serikali kulikuwa kumeenea.

## Sehemu ya 1. Kuheshimu Uadilifu wa Mtu, Ukiwemo Uhuru Kutokana na:

### a. Kuharibu Maisha bila Sababu za kimsingi na Mauaji Mengine Haramu au Mauaji yanayosababishwa na Siasa

Hakukuwa na ripoti kwamba serikali au mawakala wake walitenda mauaji ya kiholela au haramu.

Mwezi wa Juni, John Lucas Lihambalimu, afisa wa chama cha upinzani cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) huko Morogoro, alipigwa risasi kichwani na watu wasiojulikana ambao walivamia nyumba yake. Watu watatu walikamatwa kuhusiana na kifo chake.

**b. Kutoweka**

Mnamo mwaka 2017 mwandishi wa habari wa Mwananchi Communication, Azory Gwanda, alitoweka katika Wilaya ya Kibiti iliyopo Mkoa wa Pwani alipokuwa akiripoti kuhusu mauaji yasiyokuwa na maelezo katika eneo hilo na hakuwa amepatikana. Baadhi ya wafuatiliaji wa vyombo vya habari na asasi za kiraia walidai kwamba huenda Gwanda alinyamazishwa kwa sababu ya kuripoti habari za mada nyeti ya usalama. Mnamo Julai 10, Waziri wa Mambo ya Nje, Palamagamba Kabudi alielezea katika mahojiano na BBC kwamba Gwanda alikuwa amekufa; hata hivyo, baadaye waziri huyo aliikana taarifa yake. Serikali haikufanya juhudi zozote zinazojulikana kuchunguza kutoweka kwa Gwanda, wala hakuna ripoti ya kukamatwa kwa mtu yeyote kuhusiana na kutoweka kwake.

**c. Mateso na Vitendo Vingine vya Kikatili, Kinyama, au Udhalilishaji au Adhabu**

Katiba inakataza vitendo kama hivyo; hata hivyo, sheria haionyeshi kizuizi hicho cha kikatiba wala kufafanua mateso. Kulikuwa na ripoti kwamba maafisa wa polisi, walinzi wa magereza, na wanajeshi waliwanyanyasa, kuwatishia, na kuwatendea vibaya raia, watuhumiwa wa uhalifu, na wafungwa. Dhuluma hizo mara nyingi zilihusisha vipigo.

Mnamo Mei 4, Mdude Nyagali, mkosoaji wa Rais Magufuli, alitekwa nyara huko Mbozi, Songwe, na wanaume waliobeba silaha na kujifunika nyuso. Siku tano

baadaye alipatikana akiwa amepigwa na hakuwa na fahamu katika kijiji kimoja karibu na Mbeya. Kuachiliwa kwake kulitokea baada ya malalamiko ya umma na kampeni kubambe mtandaoni ikiwa na hashtagi #BringBackMdudeAlive.

Sheria inaruhusu kuchapa viboko. Maafisa wa serikali za mitaa na mahakama mara nyingi walitumia kuchapa viboko kama adhabu kwa wahalifu vijana na watu wazima. Kuchapa viboko na adhabu nyingine za kutandikwa pia zilitumiwa kwa kawaida mashuleni.

Mnamo Agosti 2018 mwanafunzi wa miaka 13 kutoka Mkoa wa Kagera, ambaye kwa makosa alituhumiwa kwa wizi, alikufa baada ya kupigwa vikali na mwalimu. Mnamo Oktoba 2018 kesi ilianza mahakamani dhidi ya waalimu wawili, ambao wote walishutumiwa kwa kumuua mwanafunzi huyo. Mnamo Machi 6, mahakama ilitoa adhabu ya kifo kwa mmojawapo wa walimu, Respicius Patrick, baada ya kumkuta na hatia ya mauaji, huku mwalimu wa pili akiachiliwa huru.

Mnamo Oktoba kanda ya video ilisambaa mtandaoni ikimwonyesha mkuu wa mkoa (RC) wa Mbeya akiwachapa viboko zaidi ya wavulana 12 waliokuwa wamelala chini. Hiyo ilikuwa adhabu kwa sababu ilidaiwa kwamba baadhi ya wavulana walichoma mabweni yao baada ya simu zao mkononi kunyang'anywa. Rais Magufuli alimpongeza RC huyo kwa adhabu hiyo, na kusema kwamba wanafunzi hao walipata walichostahili.

## Hali ya Magereza na Vituo vya Mahabusu

Hali ya magereza iliendelea kuwa mbaya na kutishia maisha. Uhaba wa chakula, msongamano, usafi duni wa vyoo, na huduma duni za afya vilikuwa vimeshamiri.

Hali ya Mazingira: Magereza yaliendelea kuwashikilia wafungwa kuliko uwezo wake. Kwa mfano, mnamo Julai, Rais Magufuli alitembelea Gereza la Butimba na kugundua kwamba lilishikilia zaidi ya wafungwa 1,000 ingawa lina uwezo wa kushikilia wafungwa 900 tu. Mahabusu pamoja na wafungwa waliopatikana na hatia walishikiliwa pamoja. Waliopatikana na hatia hawakutengwa kulingana na

kiwango cha makosa yao au umri wao. Baada ya ziara ya rais kwenye Gereza la Butimba, wafungwa 300 walipewa kifungo cha nje. Bodi ya Taifa ya Parole iliendelea kuwasamehe wafungwa kama njia ya kupunguza msongamano, na wafungwa 648 walipewa kifungo cha nje mnamo miaka mitatu iliyopita. Wakati huo huo, wakati wa urais wake, Magufuli amewapa wafungwa 3,530 kifungo cha nje, akiendeleza utamaduni wa kuwasamehe wafungwa mnamo kila sherehe za Siku ya Muungano tarehe 26 Aprili. Tarehe 9 Desemba, Siku ya Uhuru wa Tanzania, Rais Magufuli aliwasamehe wafungwa 5,533 na kuamuru waachiwe huru siku iliyofuata.

Mamlaka ziliwashikilia watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nane pamoja na watu wazima katika magereza kadhaa kutokana na uhaba wa vifaa vya kuweka watu kizuizini. Mnamo mwaka huo idara huru ya serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), ilizuru baadhi ya magereza na majengo yaliyoteuliwa kwa ajili ya kuweka watu kizuizini. Rasimu ya ripoti ya CHRAGG kuhusu hali ya magereza, hata hivyo, ilikuwa bado haijawekwa hadharani na ilikuwa inafanyiwa marudio na kuhakikiwa na Wizara ya Katiba na Sheria.

Taarifa kuhusu kuenea kwa vifo magerezani hazikupatikana.

Dhuluma za kimwili kwa wafungwa zilikuwa za kawaida. Kwa mfano, mfungwa wa kisiasa ambaye pia ni mbunge na upinzani, Peter Lijualikali, alisema alipigwa baada ya kuhukumiwa alipokuwa gerezani mwaka 2017.

Wafanyakazi wa magereza waliripoti uhaba wa chakula na maji, ukosefu wa umeme, mwanga usiotosha, na uhaba wa vifaa vya tiba. Magereza hayakupashwa joto, lakini iliripotiwa kwamba wafungwa waliokuwa katika mikoa baridi ya nchi walipokea mablanketi na masweta. Usafi wa mazingira haukutosha. Mnamo mwezi wa Julai 2018 Rais Magufuli hadharani alimwambia kamishna mkuu wa magereza kwamba serikali haitawapatia tena wafungwa chakula na kwamba wanapaswa kulima chakula chao wenyewe. Ingawa baadhi ya magereza bado yaliwapatia wafungwa chakula, Wizara ya Mambo ya Ndani iliripoti kwamba wafungwa walikuwa wakilima ardhi ili kupanda chakula chao wenyewe. Wafungwa wengine

waliripoti kutopokea chakula kutoka kwa mamlaka za magereza, huku wakitegemea tu kile ambacho walipewa na ndugu zao. Mwezi wa Machi, Rais Magufuli aliyataja magereza 10 kwa ajili ya mkakati wa uzalishaji wa kilimo. Mwezi Mei serikali ilizindua Bodi ya Uzalishaji Mali ya Jeshi la Magereza kuhakikisha kwamba magereza yana chakula cha kutosha kutoka kwenye miradi yao wenyewe. Zaidi ya hayo, magereza yameendelea kulima mamia ya eka za mazao ya chakula. Kwa mfano, gereza la Kitee lilima eka 282 za maharage, huku gereza la Songwe likilima eka 1,853 za mahindi.

Huduma za tiba hazikuwa za kutosha. Wasiwasi za kawaida za kiafya zilikuwa malaria, kifua kikuu, VVU/UKIMWI, matatizo ya kupumua, na magonjwa yaliyohusiana na usafi duni wa mazingira. Zahanati za magereza zilitoa kiasi kidogo cha matibabu, na marafiki na jamaa wa wafungwa kwa jumla walilazimika kutoa dawa au fedha za kuzinunua dawa. Usafiri wa kwenda kwenye vituo vya afya na hospitali ulikuwa mdogo. Kwa kuongeza, mara kwa mara maombi yalikumbwa na urasimu, ambao ulipelekea ucheleweshaji zaidi wa wafungwa kupata fursa ya huduma ya afya pale zilipotakiwa. Ingawa madaktari walifanya ukaguzi wa kawaida katika zahanati za magereza, hawakuwa na vifaa vya upimaji au upatikanaji dawa ya kutosha.

Mnamo Machi 15, wanachama wa upinzani Freeman Mbowe na Esther Matiko walikosoa hali za magereza walipoachiliwa baada ya kuwekwa kizuizini kwa miezi minne. Mbowe alisema kwamba licha ya hali ya msongamano, baadhi ya wafungwa waliambukizwa magonjwa kama vile upele baada ya kukaa kwa hadi wiki mbili bila kuoga. Matiko alisema kwamba katika gereza la wanawake wale wenye ugonjwa wa akili walifungwa pamoja na wahalifu.

Mwezi wa Agosti mwaka 2018 wafungwa wa kike waliwaambia wanachama wa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar waliowatembelea kwamba walikabiliwa na manyanyaso ya kingono na kupigwa na mamlaka gerezani.

<u>Utawala:</u> Majaji na mahakimu walifanya ziara za mara kwa mara kukagua magereza na kusikiliza matatizo kutoka wa wafungwa na mahabusu. Zaidi ya hayo,

jamaa wa wafungwa walitoa malalamiko kwa CHRAGG, ambayo ilichunguza ripoti za dhuluma, lakini matokeo ya uchunguzi huo hayakutangazwa hadharani.

Kwa upande wa Tanzania bara, wafungwa waliweza kuwasilisha malalamiko kwa mamlaka za kisheria. CHRAGG pia ilitumikia kama mchunguzi maalum. Idara ya Malalamiko ya Umma iliyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya muungano pamoja na kitengo cha uhusiano wa umma cha huduma za magereza vilijibu malalamiko ya umma na maulizo yaliyotumwa kwao moja kwa moja au kupitia vyombo vya habari kuhusu hali ya magereza.

Wafungwa na mahabusu kwa kawaida walikuwa na fursa ya kutosha kutembelewa na wageni na waliweza kuabudu kwa uhuru, kwa kiasi fulani. Waadventista Wasabato waliripoti kwamba walilazimika kufanya kazi Jumamosi. Mamlaka za bara mara nyingi ziliwahamishia wafungwa kwenye magereza tofauti bila kujulisha familia zao.

Mnamo Februari 2018 mahakama ya rufaa ilithibitisha uamuzi wa Mahakama Kuu ya Dar es Salaam kwa kubatilisha madaraka ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kupinga kupewa dhamana bila ya sababu kwa mshukiwa isipokuwa katika kesi za makosa ya uhujumu uchumi. Hilo lilipingwa kwa sababu awali DPP alikuwa amekataa kutoa idhini ya kuweka dhamana wakati wa uchunguzi; hata hivyo, chunguzi hizo zinaweza kuchukua miaka mingi. Mahakama Kuu ina mamlaka ya kufikiria maombi ya dhamana katika kesi zinazohusisha zaidi ya TZS milioni 10 ($4,400).

Mnamo Septemba 20, Rais Magufuli alitia saini sheria ya kuidhinisha mikataba ya maelezo ya washitakiwa mahakamani yenye lengo la kupunguza idadi kubwa ya kesi na kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wakati pamoja na kupunguza msongamano wa wafungwa. Ugaidi na makosa makubwa ya madawa ya kulevya hayakujumuishwa katika sheria hiyo mpya, kwa hivyo waendesha mashtaka hawana hiari ya kutia maanani mikataba ya maelezo ya washitakiwa mahakamani katika kesi za aina hizo.

Ufuatiliaji Huru: Sheria inakataza waandishi wa habari wasitembelee magereza. Kwa ujumla, upatikanaji wa wafungwa ulikuwa mgumu kwa mashirika ya nje, na mchakato wa kupata kibali cha kukutana nao ulikuwa na usumbufu.

## d. Kukamatwa au Kuwekwa Kizuizini bila ya sababu za kimsingi

Katiba inakataza kukamata na kuwaweka watu kizuizini bila sababu za msingi, ingawa wakuu wa mikoa na wilaya wana mamlaka maalum ya kutoa amri ya mtu kuwekwa kizuizini kwa hadi masaa 48 bila kufunguliwa mashtaka. Mamlaka hiyo ilitumiwa mara kwa mara kuwaweka kizuizini wanachama wa upinzani au watu walioikosoa serikali. Mnamo Julai 29, mwandishi wa habari za uchunguzi na mkosoaji wa serikali, Erick Kabendera, alikamatwa na askari kanzu ambao hawakumfahamisha mashtaka yake. Kwanza, familia yake haikujulishwa alikuwa amepelekwa kituo gani cha polisi. Baada ya kukaa kizuizini kwa siku saba, Kabendera alishtakiwa kwa makosa ya utakatishaji fedha. Mnamo Desemba alibaki gerezani baada ya kesi yake kuahirishwa mara kadhaa kwa misingi kwamba uchunguzi wa mahakama haukukamilishwa.

Sheria inawaruhusu watu waliokamatwa au waliowekwa kizuizini, bila kujali kama ni kwa kosa la jinai au kwa sababu nyingine, haki ya kupinga mahakamani uhalali wa sheria au aina holela ya kukamatwa kwao bila ya sababu ya msingi na kuweza kuachiliwa mara moja na kulipwa fidia ikigunduliwa kwamba waliwekwa kizuizini kinyume cha sheria. Sheria, hata hivyo, inataka kwamba kesi ya madai lazima ifunguliwe mahakamani ili kutoa changamoto ya aina hiyo, na hilo lilifanyika mara chache sana.

Uhuru wa mahakama unawaruhusu watu binafsi kutoa changamoto kwa maafisa wa serikali. Kwa mfano, mwezi Machi, Mdude Nyagali aliwasilisha mashtaka ya uovu dhidi ya kamanda wa polisi wa mkoa wa Mbeya na mwanasheria mkuu baada ya yeye kushinda kesi ya uchochezi mnamo Novemba mwaka 2018.

## Taratibu za Kukamata na Jinsi ya Kuwatendea Mahabusu

Kwa upande wa bara, sheria inahitaji kwamba ukamataji kwa makosa mengi ya jinai, isipokuwa makosa ya jinai yaliyotendwa mbele ya afisa wa polisi, ukamataji huo ufanywe kwa kutumia hati ya kukamata kulingana na ushahidi wa kutosha; hata hivyo, mamlaka hazikufuata sheria kila mara. Polisi mara nyingi waliweka watu kizuizini bila idhini ya kisheria. Sheria pia inataka kwamba mtu aliyekamatwa kwa uhalifu, isipokuwa mtu aliyewekwa kizuizini kwa sababu ya usalama wa taifa, ashtakiwe mbele ya hakimu mnamo masaa 24 ya kukamatwa, ukiondoa wikiendi na sikukuu, lakini mamlaka hazikufuata matakwa hayo kila mara. Kwa mfano, wakati Erick Kabendera alipokamatwa Julai 29, familia yake haikujua ni kituo gani cha polisi alikopelekwa na alikuwa akishikiliwa kwa mashtaka gani. Kwa kawaida mamlaka ziliwajulisha mahabusu mara moja kuhusu mashtaka dhidi yao, lakini kulikuwa na matukio kadhaa ambapo haikufanyika hivyo. Kulikuwa na ripoti za polisi kutumia mchakato mfululizo wa kuwaachilia watu na mara moja kuwakamata tena ili waweze kubaki chini ya ulinzi huku polisi wakikamilisha uchunguzi wao na kuandaa taarifa zilizohitajika kwa mshukiwa kushtakiwa. Pia kulikuwa na ripoti za polisi kuweka watu binafsi kizuizini bila mashtaka kwa muda mfupi kutokana na maagizo ya mamlaka za ndani.

Sheria hairuhusu dhamana kwa washukiwa katika kesi zinazohusisha mashtaka ya mauaji, uhaini, ugaidi, madawa, wizi wa kutumia silaha, biashara haramu ya binadamu, utakatishaji fedha na uhalifu mwingine wa kiuchumi, au makosa mengine ambapo mshukiwa huenda akaibua hatari kwa usalama wa umma. Katika baadhi ya kesi mahakama ziliweka masharti makali kwenye uhuru wa kusafiri na kujumuika pale zilipotoa dhamana. Katika mahakama za mwanzo na za wilaya, mara nyingine watu waliwahonga maafisa kutoa dhamana. Wabunge mara nyingine walimhonga DPP ili kumshinikiza katika utendaji wa kazi yake. Sheria inawapa washukiwa haki ya kuwasiliana na mwanasheria au kuzungumza na wanafamilia, lakini mara nyingi polisi walishindwa kuwajulisha mahabusu juu ya haki hiyo. Washtakiwa na washukiwa maskini walioshtakiwa kwa mauaji au uhaini huenda wangewasilisha maombi kwa msajili wa mahakama kuomba wapatiwe uwakilishi wa kisheria. Uwezo wa kupata mwanasheria haraka mara nyingi uliathiriwa na ukosefu wa mawakili katika maeneo ya vijijini, ukosefu wa mifumo ya mawasiliano na miundombinu, na washtakiwa kutojua kuhusu haki zao. Kwa

sababu hiyo, washtakiwa walio wengi wa uhalifu hawakuwakilishwa na mwanasheria, hata kwa makosa makubwa yaliyofikishwa mbele ya mahakama kuu. Serikali mara nyingi haikutoa taarifa kwa ubalozi wakati raia wa kigeni walipokamatwa na haikutoa msaada wa haraka wa kuwasiliana na ubalozi ilipoombwa kufanya hivyo.

Serikali ilifanya uchunguzi fulani magerezani ili kutambua na kusaidia waathiriwa wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; hata hivyo, uchunguzi haukuwa wa kina, kukiwa na uwezekano wa kuwaacha waathiriwa wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu bila kutotambuliwa katika vituo vya mahabusu. Mnamo mwaka 2018 serikali iliripoti kwamba kulikuwa na Waethiopia 1,200 katika vituo vya mahabusu, baadhi yao inawezekana walikuwa waathiriwa wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Mnamo Juni na Julai, kwa maombi ya ubalozi wa Ethiopia, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) lilithibitisha raia 1,354 wa Ethiopia katika magereza 27 katika mikoa 20. Miongoni mwa wahamiaji alikuwemo mwanamke mmoja na watoto 219 waliokuwa chini ya umri wa miaka 18. Mnamo mwaka huo Idara ya Uhamiaji, kwa ushirikiano na IOM, ilisaidia wahamiaji 573 wa Pembe ya Afrika kurudishwa na kuwarejeshwa makwao kwa hiari. Kati ya Januari 2015 na Juni, IOM ilisaidia kuwarejesha kwa hiari wahamiaji 1,406 wa Ethiopia wasio wa kawaida. Raia wa Ethiopia waliobaki gerezani ama walikuwa wamewekwa mahabusu (rumande), walipatikana na hatia, au walikuwa awali wamepatikana na hatia lakini hawakuachiliwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kuwafukuza nchini.

Ukamataji Bila Sababu za Msingi: Kulingana na sheria rais anaweza akaamuru kukamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda usiojulikana bila ya dhamana mtu yeyote anayeonekana kuwa hatari kwa utulivu wa umma au usalama wa taifa. Serikali lazima iwaachie huru wafungwa kama hao ndani ya siku 15 au kuwajulisha sababu za kuendelea kuwekwa kizuizini. Sheria pia inaruhusu mahabusu kuhoji misingi ya kuwekwa kizuizini katika vipindi vya siku 90. Serikali ya bara ina madaraka mapana ya ziada ya kuweka watu kizuizini kwa mujibu wa sheria, ikiruhusu wakuu wa mikoa na wilaya kumkamata na kumweka kizuizini kwa masaa 48 mtu yeyote anayeonekana “kuvuruga utulivu wa umma.”

Mahabusu Kabla ya Kushtakiwa: Ukamataji mara nyingi unatangulia uchunguzi, na washukiwa mara nyingi walibaki mahabusu kabla ya kushtakiwa--inayojulikana kama “rumande”--kwa miaka mingi kabla ya kushtakiwa, kwa kawaida bila kupewa muamana kwa kuwekwa kizuizini wakati hukumu ilipotolewa. Hakuna saa ya kuendesha kesi kwa haraka au kikomo cha sheria. Waendesha mashtaka hupata maahirisho ya kesi kutokana tu na madai ya ujumla kwamba uchunguzi bado haujakamilika. Kwa mujibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, takriban asilimia 50 ya idadi ya watu waliopo magerezani ilijumuisha mahabusu waliokuwa wakisubiri kesi zao kusikilizwa. Mahabusu walioshtakiwa kwa masuala ya uhalifu kwa kawaida walisubiri miaka mitatu minne kwa kesi zao kusikilizwa kutokana na uhaba wa majaji wa kusikiliza kesi, bajeti ya isiyotosha ya mahakama, na muda mrefu mno uliotakiwa kukamilisha uchunguzi wa polisi.

**e. Kunyimwa Fursa ya Kufunguliwa Mashtaka ya Haki na Uwazi**

Katiba inaruhusu idara ya mahakama huru, lakini vitengo vingi vya idara ya mahakama viliendelea kukabiliwa na uhaba wa fedha, rushwa, utendaji mbaya (hasa katika mahakama za chini), na ushawishi wa watendaji wa serikali. Majaji wote na maafisa wakuu wa mahakama ni wateule wa kisiasa wa rais. Kulazimika kusafiri mbali sana kwenda kwenye mahakama kunasababisha vikwazo vya usafiri na kifedha ambavyo vinazuia upatikanaji wa haki kwa watu vijijini. Kuna majaji wachache chini ya wawili kwa kila kundi la watu milioni moja. Makarani wa mahakama waliripotiwa kuendelea kula rushwa ili kufungua kesi, au kuficha au kupoteza jalada la waliotuhumiwa kwa uhalifu. Mahakimu wa mahakama za mwanzo mara chache walikula rushwa ili kufanya maamuzi ya kesi.

Asasi za kiraia (CSOs) na wanasiasa walitegemea mahakama kupinga uamuzi wa serikali. Kwa mfano, mwezi Mei Mahakama Kuu ya Dar es Salaam ilibatilisha kipengele cha katiba ambacho kiliwapa mamlaka wateuliwa wa rais kusimamia uchaguzi. Hilo lilikuwa muhimu kwa sababu asilimia 80 ya maafisa wanaosimamia uchaguzi ni wanachama wa chama tawala. Kwanza, hatua hiyo iliashiria kuwa mahakama ilitoa njia ya kukipinga chama tawala, lakini matokeo ya uamuzi

yaliyotolewa na mahakama hayakutekelezwa. Licha ya hayo mnamo Oktoba 16, Mahakama ya Rufaa, mahakama iliyo ya juu nchini, ilibatilisha uamuzi wa mwezi wa Mei wa Mahakama Kuu.

Mnamo Septemba 20, Mahakama Kuu ya Dar es Salaam ilimsimamisha Fatma Karume kufanya kazi za kisheria kuhusiana na kesi ambayo ilihoji uteuzi wa Adelardus Kilangi kama mwanasheria mkuu. Kesi iliwasilishwa na Ado Shaibu wa ACT - Wazalendo na mshtakiwa ni Rais John Magufuli. Mahakama ilimsimamisha Karume kufanya kazi ya uanasheria upande wa bara juu ya madai ya mwenendo mbaya, ikielezea kuwa hoja zake za maandishi zilikuwa “hazifai.”

**Taratibu za Mashtaka**

Sheria inatoa haki ya kufunguliwa mashtaka ya haki na uwazi, lakini mfumo dhaifu wa mahakama mara nyingi ulishindwa kulinda haki hiyo. Kesi zote zinaendeshwa na majaji; hakuna kesi zinazoendeshwa na baraza la waamuzi. Kesi haziendeshwi moja kwa moja kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Badala yake, kesi huenda ikaanza siku moja, ikaachwa kwa muda usiojulikana, na kuanza tena mara kadhaa baada ya hapo. Kutokana na hali hiyo, kesi mara nyingi hazikuendeshwa kwa ufanisi na ziliweza kudumu kwa miezi au hata miaka. Mwaka 2016 Rais Magufuli alidai kuwepo na mageuzi ya mahakama, huku akielezea kuwa mahakama ni muhimu sana kwa uwekezaji wa kigeni na ukuaji wa uchumi. Kwa msaada wa Benki ya Dunia, mwaka 2016 mahakama ilianzisha mradi wa miaka mitano, *Citizen-Centric Judicial Modernization and Justice Service Delivery Project,* ambayo inawaruhusu mawakili kuandikisha kesi zao katika kanzidata ya mtandao.

Sheria inaruhusu dhana ya kutokuwa na hatia, na kiwango cha kupatikana na hatia katika kesi za jinai ni “hadi kosa lithibitishwe.” Katika kesi nyingi mamlaka ziliwajulisha kinaganaga mahabusu kuhusu mashtaka dhidi yao mara walipopelekwa kwenye kituo cha polisi. Kwa kawaida mashtaka yaliwasilishwa kwa Kiswahili au Kiingereza pamoja na ukalimani kutolewa pale ilipowezekana. Kwa kiasi kikubwa kesi za jinai ziliendeshwa wazi kwa umma na kwa vyombo vya

habari. Washtakiwa wana haki ya kuwepo mahakamani wakati kesi zao zinaposikilizwa. Mahakama zinazoendesha kesi kwa faragha (kwa mfano, katika kesi za usafirishaji dawa za kulevya na makosa ya kingono yanayowahusisha watoto), kwa ujumla zinatakiwa kutoa sababu za kuendesha kesi hizo kwa faragha. Katika kesi zinazohusisha ugaidi, sheria inaelezea kwamba kila mtu, isipokuwa watu wanaohusika, anaweza kutolewa katika shughuli za mahakama na mashahidi wanaweza kusikilizwa kwa utaratibu maalumu kwa ajili ya kuwalinda.

Sheria inatoa msaada wa kisheria katika kesi kubwa za jinai, ingawa kiuhalisia wale walioshtakiwa kwa mauaji na uhaini tu ndio walipewa wawakilishi wa bure. Washtakiwa wengine wengi hawakuweza kumudu uwakilishi wa kisheria na walijiwakilisha wenyewe mahakamani. Washtakiwa katika masuala ya kesi za jinai wana haki ya kujichagulia uwakilishi wa kisheria. Kiutendaji uwakilishi wa kisheria haukupatikana kwa washtakiwa wasiokuwa na uwezo wa kulipa. Mashirika yasiyo ya kiserikali [NGOs] yaliwakilisha baadhi ya washtakiwa maskini katika miji mikubwa, kama Dar es Salaam na Arusha. Kwa mfano, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kinatoa huduma za bure za kisheria kinapoombwa kwa sababu mawakili wake wanahimizwa kuchukua angalau kesi moja ya bure kwa mwaka.

Visiwani Zanzibar serikali mara nyingine iliandaa watetezi wa umma katika kesi za kuua bila ya kukusudia. Sheria inakataza wanasheria wasifike au kuwatetea washtakiwa katika mahakama za mwanzo ambazo maofisa wanaoziongoza si mahakimu wenye shahada. Makundi ya haki za binadamu yalikosoa kesi zilizoripotiwa ambapo wanasheria waliojaribu kuwakilisha wateja katika kesi nyeti walitishiwa kukamatwa.

Mamlaka daima hazikuwapa mahabusu muda wa kutosha wa kutayarisha utetezi wao, na upatikanaji wa vifaa vya kutosha ulikuwa mdogo. Washtakiwa wana haki ya kupata ufasiri wa bure kama ni lazima kuanzia wakati waliposhtakiwa mpaka mwisho wa rufaa zote. Washtakiwa au mawakili wao wana haki ya kukabiliana na mashahidi wa upande wa mashtaka na haki ya kuwasilisha ushahidi na mashahidi kwa niaba ya mshtakiwa. Waendesha mashtaka, hata hivyo, hawana wajibu wa

kutoa taarifa katika kesi za jinai, na mara nyingi utetezi haujui ushahidi ambao mwendesha mashtaka atategemea wakati kesi itakapoanza. Washtakiwa hawakulazimika kutoa ushahidi au kukiri kosa.

Washtakiwa wote walioshtakiwa kwa makosa ya madai au jinai, isipokuwa wale waliofikishwa mbele ya mahakama za Kadhi huko Zanzibar (mahakama za desturi za Kiislamu ambazo zinasuluhisha masuala ya talaka na urithi), wanaweza kukata rufaa juu ya maamuzi kwenye mahakama husika Tanzania bara na Mahakama za Juu za Zanzibar. Washtakiwa wote wanaweza kukata rufaa juu ya maamuzi kwenye Mahakama ya Rufaa ya muungano.

Wataalamu wa sheria walikosoa utaratibu wa polisi kuchukua nafasi ya waendesha mashtaka kwa sababu ya hatari kwamba polisi huenda wakavuruga ushahidi katika kesi za jinai. Wizara ya Katiba na Masuala ya Sheria ya Tanzania bara iliendelea kuajiri na kutoa mafunzo kwa waendesha mashtaka wa serikali ili kushughulikia kesi zote za bara, ingawa uhaba wa wafanyakazi uliendelea.

**Wafungwa wa Kisiasa na Mahabusu**

Wanasiasa kadhaa wa upinzani na watu binafsi waliokosoa serikali walikamatwa au kuwekwa kizuizini mnamo mwaka huo. Watu hao kwa kawaida walishtakiwa kwa uhaini, uchochezi, au kukusanyika kinyume cha sheria. Kwa mfano, wabunge wawili wa upinzani, Freeman Mbowe na Esther Matiko wa CHADEMA, walitumikia miezi minne jela baada ya mahakama kufuta kiholela dhamana yao mwezi wa Novemba 2018. Katika rufaa Mahakama Kuu ya Dar es Salaam, hata hivyo, ilitoa uamuzi kwamba ufutaji huo wa dhamana ulikuwa batili, na hivyo waliachiliwa mwezi Machi. Mbowe na Matiko walikuwa sehemu ya kundi la wanachama tisa wa CHADEMA walioshtakiwa mwaka 2018 kwa makosa 11 ya jinai, yakiwemo njama, uhaini, na kuchochea kutendwa kwa makosa. Kesi ilikuwa haijamalizika, wakati timu ya upande wa utetezi ilipoanza uchunguzi wake Septemba 16.

**Taratibu za Mahakama Kuhusu Madai na Masuluhisho**

Watu wanaweza kuwasilisha mahakamani kesi za kudai fidia kutokana na uharibifu au ukiukwaji wa haki za binadamu na wanaweza kukata rufaa kwa hukumu hizo kwenye Mahakama ya Rufaa ya bara na mahakama nyingine za mikoa. Taratibu za mahakama za kiraia, hata hivyo, mara kwa mara zilikwenda polepole, hazikufanya kazi vizuri, na fisadi. Watu binafsi na wale wa taasisi zenye hadhi ya uangalizi wana haki ya kuwasilisha malalamiko kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) imekuwa njia inayopendelewa kufikisha kesi za haki za binadamu kwa sababu inakubali kesi na kupunguza mzigo kwa mahakama za ndani. Kwa mfano, kesi inayohusu kufukuzwa kwa wanavijiji kulikoongozwa na serikali mwaka 2017 huko Loliondo ilifikishwa mbele ya EACJ mnamo Septemba 2018; EACJ ilitoa uamuzi ikikubaliana na wanavijiji. Utekelezaji wa uamuzi huo, hata hivyo, bado haujafanyika. Kwa mujibu wa shahidi, watu walipigwa kila siku wakati walipopeleka ng'ombe zao kupitia eneo la hifadhi ili kufikia ardhi ya malisho. Mwezi Agosti mkuu wa wilaya ya Ngorongoro alituma ujumbe kwa Wamasai wote katika kijiji cha Loliondo kwamba lazima waondoke mnamo siku 21 au watafute mahali pengine pa kuishi.

## f. Kuingilia Kiholela au Kinyume cha Sheria katika Faragha, Familia, Nyumba, au Mawasiliano

Kwa ujumla sheria inapiga marufuku vitendo kama hivyo bila ya hati ya upekuzi, lakini serikali mara nyingi haikuheshimu marufuku hizo. Ingawa mahakama pekee ndizo zinaweza kutoa hati za upekuzi, sheria inaidhinisha upekuzi wa watu na maeneo yenye majengo bila ya hati ya upekuzi kama ni lazima ili kuzuia kupotea au uharibifu  wa ushahidi au kama mazingira ni mabaya na ya dharura. Wamiliki wa mtandao wa kijamii JamiiForums walikabiliwa na kesi kwa shutuma za kulizuia jeshi la polisi kufanya uchunguzi, kwa ukiukaji wa Sheria ya Uhalifu wa Mitandao. Polisi hawakuwa na hati ya upekuzi lakini bado waliomba anwani za IP za watumiaji wa mtandao. Wamiliki walidai kwamba ombi hilo lilikuwa uvunjaji wa faragha. Kesi iliendelea hadi mwishoni mwa mwaka jana.

Sheria inayohusiana na ugaidi inawaruhusu maofisa wa polisi wa cheo cha mrakibu msaidizi wa polisi au mkuu wa kituo cha polisi kufanya upekuzi bila ya hati ya upekuzi katika kesi fulani za haraka, lakini hakukuwa na ripoti kwamba kezi hizo zilitokea.

Iliaminika kwa kiasi kikubwa kwamba mawakala wa serikali walifuatilia simu na mawasiliano ya baadhi ya raia na wakazi wa kigeni. Hali halisi na kiwango cha ufuatiliaji huo havikujulikana. Mwezi wa Julai kulikuwa na mazungumzo ya simu za mkononi yaliyovuja ya viongozi wa chama tawala Chama cha Mapinduzi (CCM) ambao walikuwa wakihoji majadiliano ya ndani ya CCM. Abdulrahman Kinana, Nape Nnauye, na Benard Membe waliilaumu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mvujo huo. Katika mahojiano ya Julai 18 ya gazeti la *Mwananchi,* mkurugenzi mtendaji wa TCRA, James Kilaba aliiweka mamlaka mbali na uvumi wa habari iliyovuja pia kuwa na uwezo wa kuweza kurekodi mawasiliano katika simu binafsi.

## Sehemu 2. Heshima kwa Uhuru wa Kiraia, Ukiwemo:

### a. Uhuru wa Kujieleza, Ukiwemo wa Vyombo vya Habari

Katiba inaruhusu uhuru wa kuzungumza lakini haikuweka wazi uhuru wa vyombo vya habari. Kulikuwa na adhabu za kihalifu kwa kashfa.

Uhuru wa Kujieleza: Kuikosoa serikali hadharani kulisababisha kutolewa adhabu kwenye baadhi ya kesi. Mamlaka zilitumia Sheria ya Makosa ya Mtandao kufungua mashtaka ya jinai dhidi ya watu walioikosoa serikali kupitia aina mbalimbali za vyombo vya habari vya elektroniki. Mwezi wa Machi 2018 Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) zilianza kuwa sheria, zikihitaji TCRA kuthibitisha wanablogu na watumiaji wote wa majukwaa ya mtandaoni kupitia kwa mchakato wa kupata leseni.

Mnamo Julai 19, wanafunzi watatu kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania walihukumiwa kwa makosa ya kusambaza picha kupitia

makundi ya WhatsApp zikionyesha Rais Magufuli akiwa amevaa hijabu. Wanafunzi walihukumiwa miaka minne jela.

Waandishi na Vyombo vya Habari, Vikiwemo vya Mitandao: Vyombo huru vya habari vilivyopo Tanzania bara vilikuwa hai na kwa ujumla vilielezea maoni tofauti, ingawa vyombo vya habari mara nyingi vilijifanyia udhibiti wao wenyewe ili kuepuka migogoro na serikali.

Kusajili au kupata leseni ya vyombo vipya vya habari, yaani magazeti na radio kuliendelea kuwa kugumu. Usajili wa magazeti ulikuwa kwa hiari ya msajili wa magazeti katika wizara ya habari kwa pande zote mbili za bara na Zanzibar. Mchakato wa kupata leseni ya utangazaji kutoka kwa TCRA ulichukua wastani wa miezi sita hadi mwaka mmoja, na TCRA iliweka masharti kuhusu eneo la matangazo. TCRA inatoza ada za lazima za usajili na za kila mwaka kwa vituo vya radio vya biashara na kijamii. Mfumo huo wa ada unadhuru sana uwepo na uumbaji wa vituo vidogo vya redio vya kijamii.

Mnamo Februari 27, serikali ilisimamisha uchapishaji wa gazeti la Citizen na tovuti kwa muda wa siku saba, baada ya kuchapisha habari iliyokuwa na kichwa cha habari "Fuatilia kwa Karibu Kuanguka kwa Shilingi, Wataalamu Watahadharisha." Mkurugenzi wa habari alishutumu kwamba Citizen ilichapisha habari za uongo na za kupotosha kuhusu kushuka kwa thamani ya sarafu ya nchi.

Agosti 22, Joseph Gandye, mwandishi wa habari za uchunguzi wa televisheni ya Watetezi alikamatwa kwa "kusambaza habari za uongo" baada ya habari yake kuhusu ukatili wa polisi huko Iringa kutangazwa. Agosti 24, aliachiliwa kwa dhamana.

Mwaka 2017 TCRA ilifafanua mahitaji ya kwamba vituo vyote vya utangazaji vipate idhini kutoka Bodi ya Filamu Tanzania kwa maudhui yanayozalishwa ndani ya nchi, ikiwemo video za muziki, filamu, katuni, namaudhui mengine ya video. Mwezi Juni serikali ilipitisha marekebisho katika Sheria ya Filamu na Uigizaji (Rekebisho 3), kuipa Bodi ya Filamu Tanzania mamlaka ya kusimamia,

kufuatilia na kuangalia kama picha za kigeni na zile za ndani, televisheni, radio na michezo ya kuigiza na matamasha mengine zimethibitishwa kwa maonyesho.

Gazeti litolewalo kila siku linalomilikiwa na serikali ya Zanzibar, Zanzibar Leo, lilikuwa na takriban usambazaji wa nakala 25,000. Kulikuwa na gazeti moja binafsi ambao hutolewa kila wiki lenye idadi ndogo ya nakala. Serikali ya Zanzibar inadhibiti vituo vya radio na televisheni inavyovimiliki. Kulikuwa na masharti ya serikali kuhusu utangazaji kwa lugha za kienyeji, na kutangaza kwa Kiswahili au Kiingereza ndiyo lugha ambazo zinatambuliwa rasmi. Vituo tisa vya radio binafsi huko Zanzibar vinafanya shughuli zake kwa uhuru, mara kwa mara yaliyomo katika vituo vya taifa vya kila siku, ni pamoja na makala ambazo zinaikosoa serikali ya Zanzibar.

Ukosefu wa fursa ya kupata habari kutoka kwa vyanzo vya serikali uliendelea licha ya mabadiliko ya Sheria ya Takwimu.

Ukatili na Unyanyasaji: Polisi waliwashambulia, kuwanyanyasa, na kuwatishia waandishi wa habari katika kipindi cha mwaka huo. Waandishi wa habari na vyombo vya habari pia vilianza kujidhibiti vyenyewe ili kuepuka kuadhibiwa na serikali. Kukamatwa kwa mwandishi wa habari za uchunguzi Erick Kabendera Julai 29 kulibainisha ukosefu wa taratibu, ikiwa ni pamoja na kunyimwa fursa ya kumfikia wakili katika hatua za mwanzo na kuwekwa kizuizini.

Mnamo Septemba 27, TCRA ilivitoza faini vituo vitatu vya televisheni vya mtandaoni -- Kwanza Television, Millard Ayo Television, na Watetezi Television – TZS milioni tano ($2,200) kila kituo na kusimamisha matangazo ya Kwanza Television kwa miezi sita. Vituo vyote vitatu vimeelezewa kuwa vilimkosoa Rais Magufuli.

Udhibiti au Masharti ya Maudhui: Sheria inaruhusu polisi kuvamia na kukamata vifaa kutoka kwa ofisi za magazeti na inamruhusu waziri wa habari “kuzuia au vinginevyo kuweka vikwazo kwa uchapishaji wa maudhui yoyote yanayohatarisha usalama wa taifa au usalama wa umma.”

Kwa mujibu wa Waandishi Wasio na Mipaka, tangu Rais Magufuli aingie madarakani mwaka 2015, sheria za kudhibiti vyombo vya habari zimekazwa, na kumekuwepo na kesi za magazeti na vituo vya radio kusimamishwa kwa muda kwa sababu ya "uchochezi."

Makala ya Septemba 3 ya *Time Magazine* kuhusu kesi za haraka sana duniani ambazo zinatishia uhuru wa habari iliwadondoa Erick Kabendera na Azory Gwanda miongoni mwa mifano.

Kibali kilihitajika ili kuripoti kuhusu shughuli za polisi au magereza, bara na Zanzibar, na waandishi wa habari walihitaji ruhusa maalum ili kuripoti mikutano ya Bunge au kuhudhuria mikutano katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Mtu yeyote analiyechapisha habari akimshutumu mwakilishi wa Zanzibar kwa kuhusika na shughuli haramu aliwajibika kulipa faini isiyopungua TZS 250,000 ($110), kifungo cha miaka mitatu, au vyote viwili. Serikali inaweza kutoza faini na kufungia magazeti bila ya onyo.

Kulikuwa na mifano ya serikali kuzuia habari, hadi kufikia magazeti na majarida ya mitandaoni. Mwezi Juni bunge lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 ambayo yaliondoa baadhi ya masharti ya uchapishaji wa habari za takwimu. Sasa inaruhusu watu binafsi na taasisi kufanya utafiti na kukusanya data; hata hivyo, Amnesty International ilieleza kwamba kwa mujibu wa marekebisho hayo, mamlaka bado zinadumisha udhibiti juu ya nani anaweza kukusanya na kuchapisha habari, pamoja na kuamua ukweli ni nini. Ingawa Benki ya Dunia ilielezea marekebisho ya Sheria ya Takwimu inaendana na kanuni za kimataifa, wafuatiliaji wengi waliendelea kujidhibiti kwa sababu ya uwezekano wa athari binafsi na za kitaalamu, ukiwemo uwezo wa serikali kutumia sheria za huduma za vyombo vya habari na uhalifu wa mtandaoni dhidi ya watu ambao huchapisha au husambaza data ambayo haiendani na ujumbe wa serikali.

Mwezi Machi EACJ ilitoa maamuzi kwa upande wa CSOs ambao walihoji Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016. NGOs tatu, Baraza la Habari

# TANZANIA

Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) waliwasilisha kesi mwaka 2017. Mahakama iligundua kwamba vifungu kuhusu uchochezi, kashfa ya jinai, na uchapishaji wa habari za uongo vinazuia uhuru wa habari na uhuru wa kujieleza na kwa hivyo vinakiuka mkataba wa EACJ.

Sheria za Maandishi ya Kashifu/Uchongezi: Sheria inaruhusu kukamata, kufungua mashtaka, na adhabu kwa matumizi ya lugha ya uchochezi, matusi, au kuaibisha katika kueleza uongozi wa nchi. Kifungu cha 36 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari cha mwaka 2016 kinachukulia kashfa kuwa tendo la uhalifu. Kashfa imefafanuliwa kama jambo lolote linaloweza kudhuru sifa ya mtu yeyote kwa kumletea chuki, madharau, au kejeli, au kupelekea kuharibu mtu katika kazi yake au biashara yake kwa dhara kwa sifa yake.

Mwezi Februari, Mbunge wa CHADEMA (MB) Halima Mdee aliitwa kuhojiwa kuhusiana na shutuma za mwaka 2017 za kumtukana rais, ambazo zilimfanya awekwe kizuizini kwa siku sita. Kesi hiyo bado iko mahakamani na imeahirishwa mpaka mwaka 2020. Mahakama imeelezea azma ya kuitupilia mbali kesi hiyo kutokana na ukosefu wa ushirikiano kutoka kwa waendesha mashtaka.

Mnamo Aprili 24, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu iliendelea na kesi ya jinai dhidi ya Mbunge wa upinzani Zitto Kabwe. Kesi inadai kwamba Zitto alitoa matamshi kadhaa ya uchochezi dhidi ya TPF, akiishutumu kwa kuua zaidi ya raia 100 huko Kigoma. Mnamo Oktoba 23, kesi hiyo ilisikilizwa  na kuahirishwa mpaka 2020.

Mnamo Machi 10, Waziri wa Mambo ya Ndani Kangi Lugola aliamuru makamanda wa polisi wa mikoa kote nchini kuwakamata viongozi wa vyama vya upinzani ambao walimtukana rais. Mnamo Septemba 26, Lugola pia aliionya CSOs dhidi ya kuitukana serikali.

Usalama wa Taifa: Mwezi Machi 2018 Kanuni za Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) zilipitishwa, zikiwataka wanaotoa maudhui ya

mtandaoni kufuatilia na kuchuja maudhui ambayo yanatishia ulinzi wa taifa au afya na usalama wa umma.

## Uhuru wa Intaneti

Serikali ilidhibiti upatikanaji wa intaneti na ilifuatilia tovuti na shughuli za intaneti. Kanuni za Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) zinakaza udhibiti wa maudhui ya mtandaoni kupitia kwa mahitaji ya usajili na ada za leseni. Wanablogu na watu wanaoendesha vikao mitandaoni, ikiwa ni pamoja na huduma za upitishaji wa data kwenye televisheni na radio mtandaoni, lazima wapate hati kutoka kwa TCRA kwa kuwasillisha maombi ya leseni yanayohitaji habari kama vile aina ya huduma zinazotolewa, makadirio ya gharama ya uwekezaji, sifa za wafanyakazi, na mipango. Zaidi ya hayo, watoa huduma wote wa mtandaoni lazima walipe ada za maombi na leseni za jumla ya zaidi ya TZS milioni mbili ($880) katika gharama za mwanzo. Leseni ni halali kwa miaka mitatu na lazima zitolewe upya kila mwaka kwa gharama ya shilingi milioni moja ($440). Gharama kubwa sana zilisababisha baadhi ya raia kuacha kublogu au kubandika maudhui katika vikao mtandaoni, yakiwemo majukwaa ya kimataifa ya mitandao ya kijamii.

Kwa mujibu wa kanuni hizo mikahawa ya intaneti lazima iweke kamera za uchunguzi ili kufuatilia watu mtandaoni. Vitu vya mtandaoni vinavyochukuliwa kuwa "vya kuchukiza, vya kukiuka maadili" au "kusababisha kero," ni marufuku, na wale wanaoshtakiwa kwa ukiukaji wa sheria wanakabiliwa na faini isiyopungua TZS milioni tano ($2,200) au hukumu isiyopungua kifungo cha miezi 12 gerezani. Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 inaharamisha uchapishaji wa habari za uongo, zinazofasiliwa kama "habari, data au ukweli unaowasilishwa kwa picha, maandiko, alama, au aina nyingine yoyote katika mfumo wa kompyuta ambapo habari, data, au taarifa kama hizo ni za uongo, udanganyifu, upotoshaji, au sio sahihi." Watu waliotoa maoni ya ukosoaji kuhusu serikali wakitumia vyombo vya habari vya elektroniki walishtakiwa chini ya sheria hiyo, hata kama matamshi yaliashiria maoni au yalikuwa ya kweli.

Mwaka 2018 Bob Wangwe alikata rufaa kwenye Mahakama Kuu ya Dar es Salaam kuhusu uamuzi wa mahakama ya Kisutu uliomkuta na hatia na kumtoza faini ya TZS milioni tano ($2,200) au kifungo cha miezi 18 kwa kuchapisha habari isiyo sahihi kwenye Facebook. Mwezi wa Machi alishinda rufaa yake. Mahakama iliamua kwamba serikali ilipaswa kuthibitisha kwamba habari iliyobandikwa mtandaoni na Wangwe ilikuwa halisi, na ilikuwa na nia gani.

Mnamo Septemba 7, Sebastien Atilio alikamatwa kwa kuchapisha habari za uongo na kufanya kazi ya uandishi wa habari bila ya kutambuliwa rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari kuhusiana na ujumbe aliotuma kwa kundi la WhatsApp linaloitwa Mufindi Media Group. Usikilizaji wa awali wa ombi la dhamana uliopangwa kufanyika Septemba 18 uliahirishwa mara kadhaa. Mnamo Oktoba 28, Atilio aliachiliwa kwa dhamana na jaji aliamuru mwendesha mashtaka wa umma kukamilisha uchunguzi mnamo siku 61 au jaji angeiondoa kesi mpaka uchunguzi ukamilike. Kesi ilikuwa bado haijaamuliwa hadi kufikia Desemba.

**Uhuru wa Kitaaluma na Matukio ya Kitamaduni**

Mwezi Juni bunge lilipitisha marekebisho kwa mara ya pili mnamo miaka miwili kwa Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, ambayo ilikuwa ikiwataka watu binafsi na mashirika kupata ruhusa kutoka kwa Taasisi ya Taifa ya Takwimu kabla ya kufanya uchunguzi, kukusanya data za utafiti, au kutangaza matokeo. Marekebisho hayo yaliondoa tishio la kufungwa gerezani kwa makundi ya asasi za kiraia kama yangechapisha habari za takwimu. Marekebisho hayo pia yanasema kwamba watu wana haki ya kukusanya na kusambaza habari za takwimu, na kuweka mfumo kwa ajili ya watu ambao wanataka kupata na/au kuchapisha data za taifa.

## b. Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika kwa Amani

**Uhuru wa Kukusanyika kwa Amani**

Serikali ilizuia uhuru wa kukusanyika na kujumuika kwa amani, ikijumuisha kupitia kwa amri zilizopigwa marufuku na mamlaka lakini hazikuwa na nguvu ya

kisheria. Serikali inataka waandaaji wa mikutano ya hadhara wapate ruhusa kutoka kwa polisi. Polisi wanaweza kukataa kutoa ruhusa kwa misingi ya usalama au ulinzi wa umma au kama anayetafuta kibali ni mwanachama wa shirika au chama ambacho hakijasajiliwa. Serikali na polisi waliendelea kubana utoaji wa vibali vya maandamano na mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa vya upinzani, NGOs, na mashirika ya kidini. Mikutano ya pekee ya kisiasa inayoruhusiwa kimsingi ni ya wabunge katika majimbo yao ya uchaguzi; washiriki wa nje, ikiwa ni pamoja na viongozi wa chama, hawaruhusiwi kushiriki. Vikwazo pia vilitumiwa kwa mikusanyiko isiyo ya kisiasa huku ikiaminiwa kuwa ilikosoa serikali.

Chama tawala cha CCM ni chama cha pekee ambacho kimeruhusiwa kisheria kufanya mikutano ya hadhara. Kinatumia mwavuli wa manifesto ya chama cha utekelezaji ili kuwafahamisha wanachama iwapo ni wakati wa kujiandikisha kupiga kura.

Vyama vya siasa vya upinzani viliendelea kunyanyaswa na kuwekwa kizuizini na utekelezaji wa sheria na havijafanikiwa kupata haki mahakamani. Kwa mfano, mnamo Mei 27, waziri wa zamani wa utalii na mali asili, Lazaro Nyalandu na wanachama wawili wa upinzani kutoka CHADEMA walikamatwa katika Wadi ya Itagio kule Singida wakati wa mkutano wa faragha. Waliachiliwa kwa dhamana siku ya pili yake, baada ya kuhojiwa na Tume ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) kwa zaidi ya masaa mawili.

Mwezi wa Julai, polisi wa Zanzibar walimkamata Seif Hamad Sharif wakati wa tukio la kumbukumbu ya miaka 10 ya maridhiano ya kisiasa huko Zanzibar. Polisi walimhoji Seif kabla ya kumuachilia na kulifuta tukio hilo.

## Uhuru wa Kujumuika

Katiba inaruhusu kuwepo uhuru wa kujumuika, na serikali kwa ujumla iliheshimu haki hiyo. Maelfu ya NGOs na jamii zilifanya kazi nchini. Vyama vya siasa vilitakiwa kusajiliwa na kukidhi mahitaji ya uanachama na mahitaji mengine. Uhuru wa wafanyakazi kujumuika ulikuwa mdogo (angalia sehemu 7.a.).

**TANZANIA**

Kwa mujibu wa International Center for Not-for-Profit Law na LHRC katika ripoti yao ya katikati ya mwaka, uhuru wa kujumuika kwa NGOs umehatarishwa na marekebisho ya sheria ya NGO, ambayo inapunguza uwezo wa NGOs kujitawala na inaruhusu kanuni nyingi mno katika sekta ya NGO. Msajili alielezea kwamba mchakato wa kubatilisha usajili ulisisitiza hitaji la NGOs kufuata sheria na kutoa uwazi na uwajibikaji katika shughuli zao. Chini ya sheria zilizopo, hata hivyo, msajili wa NGOs amepewa uwezo kamili wa kusimamisha au kufuta usajili wa NGOs, na kuacha mianya ambayo inaweza kutumiwa kuzuia upinzani na NGOs za haki za binadamu. Kwa mfano, msajili alizifuta NGOs 158 mnamo mwezi wa Agosti. Community Health Education Services and Advocacy, Kazi Busara na Hekima (KBH Sisters), na AHA Development Organization Tanzania zilifutwa eti kwa sababu ya kuendeleza vitendo katika jamii ambavyo vinakiuka maadili na utamaduni kwa sababu vilitegemeza ulinzi na haki za LGBTI. Wengine waliojiondoa walikuwa Pathfinder Green City, Hamasa Poverty Reductions (Hapore), na Hope.

Sheria inatofautisha kati ya NGOs na jamii na inatumia taratibu tofauti kuandikisha hizo mbili. Inafafanua jamii kama klabu, kampuni, ushirika, au chama chochote cha watu 10 au zaidi, bila ya kujali nia yake, na inabainisha aina maalum za mashirika ambayo hayazingatiwi kuwa jamii, kama vile vyama vya siasa. Sheria inafafanua NGOs kujumuisha mashirika ambayo madhumuni yao ni kukuza maendeleo ya uchumi, mazingira, ujamii, au utamaduni; kulinda mazingira; au kushawishi au kutetea maswala yenye maslahi kwa umma. Jamii na mashirika huenda yasifanye kazi mpaka mamlaka ziidhinishe maombi yao. Mnamo Agosti serikali ilianza zoezi la thibitisho ambalo lilitaka NGOs zote zijiandikisha tena. Usajili wa NGOs mpya ulisimamishwa mpaka Desemba 1.

Serikali mara chache ilisaijili vyama vya kijamii mnamo kipindi kilichowekwa kisheria cha siku 14. Mwezi Aprili waziri wa mambo ya ndani alieleza kwamba kuanzia Julai 2018 mpaka Machi, msajili wa vyama vya kijamii alipokea maombi 150 ya usajili, 77 kutoka kwa taasisi za kidini na 73 kutoka kwa CSOs. Msajili

alisajili maombi 69: CSOs 38 na taasisi 31 za kidini. Kati ya waombaji hao, 81 walikuwa bado wakishughulikia maombi yao.

NGOs za Zanzibar hutoa maombi ya usajili kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar. Ingawa usajili kwa jumla ulichukua wiki kadhaa, baadhi ya NGOs zilisubiri kwa miezi mingi iwapo msajili aliamua kwamba utafiti wa ziada ulihitajika.

Mwezi wa Julai NGO ilisema Zanzibar ina sera iliyopitwa na wakati ya NGO na kwamba mamlaka za mitaa haziwezi kufikia mahitaji yanayobadilika ya NGOs na shughuli kote nchini. Kwa mujibu wa baadhi ya NGOs, usalama na mashirika ya serikali yalikuwa yanaingilia kazi ya NGOs. Kwa mfano Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilisimamisha utekelezaji wa mradi wa vijana, ikielezea kwamba ilihitaji muda zaidi kuchunguza wigo wa mradi huo. Serikali, hata hivyo, inachukulia kikundi chochote cha vijana kama upinzani unaojipanga.

## c. Uhuru wa Dini

Tazama *Ripoti ya Kimataifa ya Uhuru wa Dini* ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani Kwenye www.state.gov/religiousfreedomreport/.

## d. Uhuru wa Kusafiri

Katiba inaruhusu uhuru wa kusafiri ndani ya nchi, safari za nje, uhamaji, na kuwarejesha watu makwao, na serikali kwa ujumla iliheshimu haki hizo; hata hivyo, kulikuwa na kesi za viongozi wa upinzani kuzuiliwa wasiondoke nchini.

Kusafiri Ndani ya Nchi: Wakimbizi wanawekwa katika kambi na wanaweza kukamatwa wakiondoka huko. Chini ya masharti yake makali zaidi ya kuwa mwenyeji wa wakimbizi, serikali ilipunguza mwendo wa wakimbizi na kutekeleza sera yake ya kuwepo kambini kwa masharti makali zaidi mnamo mwaka huo, kukiwemo kuwakamata wakimbizi ambao waliopatikana wakitembea nje ya kambi

bila ruhusa rasmi. Huku ikiwa vigumu kupata vibali na fursa za riziki ndani ya kambi zikiwa finyu sana, wakimbizi waliolazimika kuondoka kwenye kambi kwenda kutafuta kazi walikamatwa na polisi. Kwa kawaida watu hao walishtakiwa na kuhukumiwa na mahakama za chini kuwekwa kizuizini kwa miezi sita au kulipa faini.

Kusafiri Nje ya Nchi: Mnamo Juni 12, maafisa wa uhamiaji wa Zanzibar walimweka kizuizini kiongozi wa upinzani na mbunge Zitto Kabwe, ambaye alikuwa njiani akienda Kenya kuhudhuria kipindi cha faragha na viongozi wa chama chake cha Alliance for Change and Transparency (ACT). Wakifuata maagizo kutoka kwa PCCB kutomruhusu Kabwe kuondoka nchini kutokana na mashtaka ambayo yalikuwa yanasubiri uamuzi chini ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, maafisa wa uhamiaji walimhamishia Kabwe kwa ulinzi wa polisi. Polisi baadaye walimwachilia Kabwe lakini walimnyang'anya simu yake ya rununu na kipakatilishi chake.

Mwezi wa Februari kusafiri kwa wafanyakazi wahamiaji kwenda nje ya nchi kwa ajira kulisimamishwa kwa muda, eti ili kuipatia serikali nafasi ya kuimarisha taratibu za kulinda wafanyakazi wahamiaji.

Uraia: Hakukuwa na ripoti za kufutwa kwa uraia kwa misingi ya kiholela au kibaguzi.

## e. Watu Waliokoseshwa Makazi Ndani ya Nchi

Hakukuwa na ripoti za idadi kubwa ya watu waliokoseshwa makazi ndani ya nchi.

## f. Ulinzi wa Wakimbizi

Dhuluma Dhidi ya Wahamiaji, Wakimbizi, na Watu Wasio na Uraia: Licha ya ahadi za serikali kwamba mipaka yake ilibaki wazi kwa wakimbizi, mnamo mwaka huo maafisa walifunga mipaka kwa wakimbizi wapya waliowasili kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi. Mnamo Januari 2018

serikali ilijiondoa kutoka kwa mpango wa Umoja wa Mataifa wa Comprehensive Refugee Response Framework, ikatangaza kwamba haitatoa uraia tena kwa wakimbizi wa Burundi, na ikaelezea kwamba itawahimiza wakimbizi kurudi nyumbani. Wakati huo serikali iliihakikisha Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu wa Wakimbizi (UNHCR) kwamba itaheshimu machaguo ya wakimbizi kuhusu kama wanataka au hawataki kurudi kwenye nchi waliyotoka. Ingawa wakimbizi 75,000 wa Burundi walikuwa wamerejeshwa makwao kwa msaada kati ya Septemba 2017 na Septemba 2019, kulikuwa na visa vingi vya wakimbizi kukabiliwa na vitisho au shinikizo kutoka kwa mamlaka za Tanzania kurejea nyumbani. Baadhi ya wakimbizi ambao walishinikizwa kurudi Burundi walikuwa wakimbizi katika nchi nyingine au walirudi Tanzania.

Mwezi wa Agosti Waziri wa Mambo ya Ndani Lugola alitangaza makubaliano ya pande mbili na Burundi ya kuwarejesha nyumbani Warundi 2,000 kwa wiki, iwe kwa hiari au la. Ingawa serikali ya Tanzania baadaye ilielezea tena ahadi yake ya kuwarejesha makwao kwa hiari, UNHCR ilibaki na wasiwasi kuhusu kuthibitisha hiari ya waliorejea makwao. Zaidi ya hayo serikali ilisimamisha kwa muda machaguo ya riziki ya wakimbizi, yakiwemo kufungwa kwa biashara inayofanya kazi ndani ya kambi na masoko ya kawaida nje ya kambi ambapo wakimbizi na jamii zinazowazunguka wangeweza kubadilishana bidhaa. Kwa mujibu wa NGOs zinazofanya kazi katika kambi hizo, kulikuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia na wasiwasi mwingine kutokana na upotezaji wa riziki.

Wakimbizi waliokamatwa zaidi ya maili 2.5 nje ya kambi zao bila ya vibali maalum walikabiliwa na sheria na adhabu za kuanzia faini mpaka kifungo cha miaka mitatu gerezani. Kwa kuongezea kumekuwa na ripoti za wakimbizi kupatikana nje ya kambi na kuwekwa kizuizini, kupigwa, kuteswa, kubakwa, au kuuawa na maafisa au raia.

Mnamo Aprili 5, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yusuph Masauni aliripoti kwamba wahamiaji haramu 13,393 walikamatwa nchini. Kati ya idadi hiyo, 2,815 walishtakiwa kwa kuingia nchini kinyume cha sheria, 117 walilipa faini, na 429 walihukumiwa kifungo cha jela. Kati ya wale waliokamatwa, 6,316

walirejeshwa makwao na 1,313 waliachiliwa baada ya kuthibitisha ukaazi wao. Idara ya Uhamiaji ndio wakala wa serikali unaoongoza shughuli za kutambulisha hadhi ya wahamiaji na hatua ya baadaye. Kwa mujibu wa ripoti moja, wakulima haramu 39 kutoka nchi jirani walikamatwa katika mkoa wa Kagera.

Ukatili wa kingono na kijinsia dhidi ya wakimbizi uliendelea, yakiwemo madai dhidi ya maafisa waliofanya kazi ndani au kandokando ya kambi za wakimbizi. UNHCR ilifanya kazi na mamlaka za mtaa na wakazi katika kambi tatu za wakimbizi kuimarisha uratibu na kushughulikia ukatili, ukiwemo ukatili wa ngono, dhidi ya watu walio katika mazingira hatarishi. Mwendesha mashtaka wa umma alichunguza, akawashtaki, na kuwaadhibu wakosaji wa dhuluma katika kambi, huku NGOs za kimataifa zikitoa msaada kwa timu ya kisheria zilipoombwa na manusura. Mamlaka za mtaa na mwendesha mashtaka wa umma walishughulikia kesi nyingi za wakimbizi waathiriwa wa uhalifu na ukatili nje ya kambi. Wakazi wa kambi za wakimbizi waliteseka na ucheleweshо na pia fursa chache za kufikia mahakama, matatizo ya kawaida ambayo pia yalikabiliwa na raia.

Kurudisha Wakimbizi Kwa Nguvu katika Nchi ya Mateso: Serikali ilifunga kituo cha mwisho rasmi nchini cha kupokea wakimbizi mwaka 2018, na mwaka huo kulikuwa na ripoti za uhakika juu ya kuwarudisha kwenye mpaka pamoja na matukio ya kuwanyima fursa kwa wakongo na warundi wanaotafuta hifadhi kufuatia maombi ya kutaka ulinzi wa kimataifa katika nchi. Zaidi ya hayo wakimbizi wa Burundi ambao walisaidiwa na UNHCR mnamo mwaka huo kurudi Burundi kwa hiari, lakini wakalazimika kukimbia tena na kuomba hifadhi kwa mara ya pili, walishindwa kujisajili kwa mamlaka. Hali hiyo iliwazuia wasipate fursa ya msaada wa kibinadamu au huduma za msingi.

Upatikanaji wa Hifadhi: Sheria inaruhusu utoaji wa hifadhi au hadhi ya ukimbizi, na serikali ina mfumo imara wa kutoa ulinzi kwa wakimbizi. Kamati ya Ustahili ya Taifa inatakiwa kukutana mara kwa mara na kufanya uamuzi juu ya maombi ya hifadhi.

# TANZANIA

Licha ya sera kali ya serikali, mamlaka ziliendelea kuruhusu idadi ndogo ya walioomba hifadhi na wakimbizi kukaa mjini Dar es Salaam; kundi hilo kimsingi lilijumuisha watu wenye mahitaji ya ulinzi wa kimataifa huku wakiwasili kutoka nchi ambazo si jirani pamoja na watu wenye sababu maalum za kutoweza kukaa katika kambi za wakimbizi magharibi mwa nchi. Ingawa upatikanaji wa fursa za ajira rasmi uliendelea kuwa mdogo kwa wakimbizi wa mjini, walifurahia upatikanaji wa huduma za afya na shule za serikali. UNHCR iliendelea kuingilia kati katika kesi za wahamiaji wasio wa kawaida waliohitaji ulinzi wa kimataifa baada ya kukamatwa na mamlaka mjini Dar es Salaam au katika vituo vingine vya mjini ili kuhakikisha kwamba wahamiaji walikuwa na upatikanaji wa taratibu za hifadhi za kitaifa na walilindwa kutorejeshwa kwa nguvu kwenye nchi zao za asili.

Mnamo mwaka huo serikali na IOM ziliendelea kusaidia mafunzo ya maafisa wa utekelezaji wa sheria juu ya matumizi ya vifaa vya usajili vya kibayometriki vilivyokusudiwa kuwapa wahamiaji wasio wa kawaida msingi wa ama kurekebisha hadhi yao au kurudi kwa hiari katika sehemu zao za asili.

Nchi Salama ya Asili/ya Kupita: Hakuna sera ya makatazo ya jumla au yanayotazamiwa ya hifadhi kwa waombaji wanaowasili kutoka "nchi salama ya asili" au kupitia "nchi salama ya kupita." Maombi yote ya hifadhi yalitathminiwa kibinafsi. Kulingana na sheria, isipokuwa kama nchi ya kupita ilikuwa inakabiliwa na uvunjaji mkubwa wa amani, dai la hifadhi linaweza kukataliwa kutokana na kushindwa kuonyesha sababu yenye busara kuhusu kwa nini hifadhi haikudaiwa katika nchi ya kupita kabla ya kuingia Tanzania.

Uhuru wa Kusafiri: Masharti ya sera yaliyoweka kikomo kwa uhuru wa kusafiri na upatikanaji wa riziki wa wakimbizi yaliacha jamii ya wakimbizi kwa kiasi kikubwa ikitegemea msaada wa kibinadamu na kutolindwa dhidi ya hatari anuwai za ulinzi, ukiwemo ukatili wa kingono na kijinsia. Ukatili kati ya washirika uliendelea kuripotiwa kama aina kuu ya ukatili wa kingono na kijinsia na kuwakilisha takriban asilimia 75 ya matukio. Waangalizi walidhani kwamba kiwango hicho cha ukatili kilitokana na mazingira magumu ya kuishi katika kambi za wakimbizi, maamuzi ya mgawanyiko katika familia yalitokana na shinikizo la

serikali kuwarejea na matumizi mabaya ya vileo; kufungwa kwa masoko makubwa, ambako kulidumaza juhudi za wanawake kujitegemea; na masharti ya uhuru wa mwendo, ambayo yaliweka wanawake na wasichana katika hali ya hatari walipoondoka kambini kukusanya kuni na kutafuta vyakula vingine ili kufanya anuwai mlo wa familia zao.

Ufumbuzi wa Kudumu: Mnamo mwaka huo serikali ililenga kurejeshwa makwao na haikuunga mkono kuchanganyika katika jamii kama suluhisho la kudumu. Serikali ilidumisha shinikizo kwa wakimbizi wa Burundi kurejea Burundi, ikiendeleza kurejeshwa makwao kama suluhisho pekee la kudumu kwa wakimbizi wa Burundi. UNHCR iliendelea kusaidia kurejeshwa kwa hiari chini ya muundo wa mkataba wa pande tatu kati ya serikali za Burundi na Tanzania na UNHCR, ikisisitiza kwamba mazingira ndani ya Burundi bado hayakufaa kurejeshwa kwa idadi kubwa kwa sababu wakimbizi wengi wa Burundi bado walihitaji ulinzi wa kimataifa. Hata hivyo, mnamo Agosti serikali iliongeza shinikizo kwa wakimbizi wa Burundi kutia kujiandikisha kwa marejeo, wakikubaliana na serikali ya Burundi kurejesha kwa Warundi 2,000 kwa wiki, lakini pia ikisema kwamba wakimbizi wote wa Burundi watarejeshwa ifikapo mwisho wa mwaka huo. Serikali ilitekeleza hatua za kufanya maisha yawe magumu zaidi kwa wakimbizi, ikiwa ni pamoja na kufunga masoko yaliyotumiwa na wakimbizi pamoja na jamii ya wenyeji mwezi wa Februari na kuweka masharti ya vibali vya kutoka katika kambi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kutoka Julai 2018 mpaka Machi 28, jumla ya wakimbizi 662 wa Burundi walirudi makwao kwa hiari yao. Kwa mujibu wa UNHCR, karibu wakimbizi 75,000 wa Burundi wamerudi nyumbani kwa msaada tangu mwaka 2017. Serikali iliwapa uraia wakimbizi 162,000 wa zamani wa Burundi mnamo mwaka 2014-15. Mnamo mwaka huo wakimbizi 1,350 kutoka DRC na 82 kutoka nchi nyingine walipewa makazi katika nchi nyingine.

### g. Watu Wasio na Uraia

Haihusiki

## TANZANIA

## Sehemu 3. Uhuru wa Kushiriki Mchakato wa Kisiasa

Katiba inawapa raia uwezo wa kuchagua serikali yao katika uchaguzi huru na wa haki ambao unafanyika kwa njia ya kura ya siri na kulingana na misingi ya usawa na haki, lakini inaliruhusu bunge kuzuia haki hiyo kama raia ana ugonjwa wa akili, alipatikana na hatia ya makosa fulani ya jinai, au anaacha au kushindwa kuthibitisha au kutoa ushahidi wa umri, uraia, au usajili kama mpiga kura. Raia wanaoishi nje ya nchi hawaruhusiwi kupiga kura. Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawajibika kwa mambo ya uchaguzi wa bara na muungano, huku Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ikisimamia uchaguzi Zanzibar.

### Uchaguzi na Ushiriki wa Kisiasa

<u>Uchaguzi wa Karibuni:</u> Nchi ilifanya uchaguzi mkuu wa karibuni kabisa wa vyama vingi mwaka 2015, ambapo rais mpya na wawakilishi wa baraza la kutunga sheria walichaguliwa. Uchaguzi wa muungano kwa kiasi kikubwa ulielezewa ulikuwa huru na wa haki, ingawa baadhi ya watu wa upande wa upinzani na asasi za kiraia walidai kwamba kulikuwepo na wizi wa kura. CCM ilinufaika na rasilimali za hali ya juu za kifedha na kitaasisi. Pia kulikuwa na ripoti kwamba matumizi ya rasilimali za umma katika kuisaidia CCM yaliongezeka, pamoja na ripoti nyingi za wakuu wa mikoa na wilaya kukifanyia kampeni chama tawala.

Katika uchaguzi wa urais mgombea wa CCM, John Magufuli, alichaguliwa kwa asilimia 58 ya kura kuchukua nafasi ya Jakaya Kikwete ambaye hakustahili kugombea muhula wa tatu. Vyama vinne vya upinzani viliungana kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi ili kumuunga mkono mgombea mmoja, ambaye aligombea kwa tiketi ya CHADEMA, kwani sheria wakati huo haikutambua miungano. Mwezi Februari sheria ya Vyama vya Siasa iliyorekebishwa ilitambua rasmi miungano. Katika uchaguzi wa bunge, CCM iliendelea kuwa na idadi kubwa sana bungeni, ikiwa na karibu asilimia 73 ya viti.

Chaguzi tofauti zilifanyika kwa muungano na kwa Zanzibar, kwa kawaida siku moja sawa, ambapo raia katika pande mbili za muungano wanawachagua viongozi

wa ndani, wanachama wa bunge la muungano, na rais wa muungano (taifa). Zaidi ya hayo, Zanzibar peke yake inamchagua rais wa Zanzibar na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Upigaji kura wa Zanzibar wa mwaka 2015 kwa kiasi kikubwa ulikuwa huru na wa haki. Kufuatia upigaji kura huo, hata hivyo, wakati hesabu ya matokeo ilipokuwa zaidi ya nusu kukamilika, mwenyekiti wa ZEC alitangaza kwamba alikuwa amefuta uchaguzi wa Zanzibar. Kwa mujibu wa katiba na sheria, tume haina mamlaka ya kufanya hivyo. Uamuzi huo ulisababisha mgogoro wa kisiasa katika visiwa hivyo vyenye utawala kiasi, huku mgombea wa upinzani akijitangazia ushindi. Uchaguzi mpya mwaka 2016 haukuwa jumuishi wala wakilishi. Uchaguzi huo mpya ulisusiwa na upinzani, ambao ulidai hautakuwa wa haki. Kufuatia uchaguzi huo mpya ZEC ilitangaza kwamba Rais Ali Mohammed Shein alikuwa ameshinda kwa asilimia 91 ya kura, huku chama tawala CCM kikichukua karibu viti vyote katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Idadi rasmi ya wapiga kura waliojitokeza ilitangazwa kuwa asilimia 68, ingawa vyanzo vingi vilikadiria idadi halisi ya wapiga kura kuwa karibuzaidi na asilimia 25.

Kati ya Novemba 2017 na Julai 13, chaguzi ndogo zilifanyika bila ya kupata fursa ya kujiandaa kwa nafasi ya diwani na viti vya bunge ambavyo viliachwa wazi kutokana na vifo, kuhama chama, kujiuzulu, au kufukuzwa kwa walioshikilia vyeo. Mara kadhaa mwanachama wa upinzani alipohamia chama tawala hatimaye aliteuliwa kama mgombea wa chama tawala kwa kiti hicho hicho ambacho mtu huyo alikiacha. Chaguzi ndogo ziligubikwa na mambo yasiyo ya kawaida, ikiwa ni pamoja na kuwanyima mawakala walioteuliwa wasifike kwenye vituo vya kupigia kura, wanachama wa chama cha upinzani kunyanyaswa na polisi, na kukamatwa bila ya sababu. Mara nyingi wagombea wa upinzani walizuiwa wasijiandikishe, na hiyo hali ilisababisha nafasi nyingi za ushindani kutangaziwa chama tawala bila ya kupingwa.

Mwezi wa Machi spika wa bunge alimuondoa mbunge wa upinzani wa CHADEMA Joshua Nassari kutoka kwa kiti chake kutokana na kutokuwepo bungeni kwa kawaida. Mahakama ilikubaliana na kuondolewa kwake Nassari alipohoji uamuzi huo. Mwezi Juni spika pia alimuondoa mbunge wa upinzani wa CHADEMA Tundu Lissu kwa kutokuwepo bungeni kwa kawaida na kushindwa

kuwasilisha kauli za kuelezea taarifa zake kwa muda muafaka. Lissu alinusurika jaribio la kuuawa mwaka 2017 na tangu wakati huo amekuwa nje ya nchi kwa matibabu. Mahakama ilitupilia mbali hoja ya Lissu ya kuondolewa kwake, na mwanachama mpya wa CCM aliapishwa Septemba 3 kuwakilisha jimbo lake la uchaguzi.

Mnamo Oktoba 16, Mahakama ya Rufaa ilifuta uamuzi wa mwezi Mei wa Mahakama Kuu ya Dar es Salaam kupiga marufuku wakurugenzi wa wilaya kusimamia uchaguzi kwa misingi kwamba usimamizi wao unakiuka marufuku ya kikatiba kuhusu vyama vya siasa kuendesha uchaguzi. Wakurugenzi watendaji wa wilaya wanateuliwa na rais kuwa kama makatibu wa mabaraza ya wilaya, na wengi ni wanachama hai wa chama tawala CCM.

Vyama vya Siasa na Kushiriki Kisiasa: Katiba inataka kwamba watu wanaogombea uchaguzi lazima wawakilishe chama cha siasa. Sheria inakataza vyama visivyosajiliwa. Kulikuwa na vyama 22 vya siasa vyenye usajili kamili na kimoja chenye usajili wa muda. Kupata usajili kamili, vyama lazima viwasilishe orodha za angalau wanachama 200 katika mikoa 10 kati ya 31 ya nchi, ikiwemo mikoa miwili kati ya mitano ya Zanzibar.

Msajili vya vyama vya siasa ndiye pekee mwenye mamlaka ya kuidhinisha usajili wa chama chochote cha siasa na anawajibika kwa kuimarisha kanuni. Mwezi Februari marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yalipanua madaraka ya msajili, hatua ambayo wabunge wa upinzani walidai itaimarisha nguvu ya utawala wa chama kimoja. Chini ya marekebisho ya sheria msajili anaweza kumpiga marufuku mtu yeyote kujihusisha na harakati za kisiasa na kuomba habari yoyote kutoka kwa chama cha siasa, zikiwemo kumbukumbu na waliohudhuria mikutano ya chama. Mwezi Machi msajili wa vyama vya siasa alitishia kukifuta chama cha ACT kwa kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa. Tishio la kukifuta lilikuja wiki moja baada ya Seif Sharif, mwanasiasa maarufu wa upinzani Zanzibar, alipotangaza kuondoka chama cha Civil United Front (CUF) na kujiunga na ACT. Wafuasi wa Sharif walichoma moto bendera za CUF wakati wa tangazo hilo, wakivunja sheria.

Sheria inavitaka vyama vya siasa kuunga mkono muungano kati ya Tanganyika (Tanzania Bara) na Zanzibar; vyama vinavyojikita katika uhusiano wa kikabila, kimkoa, au kidini vinakatazwa.

Wabunge waliadhibiwa kwa kuelezea ukosoaji wao dhidi ya serikali, ikiwa ni pamoja na hotuba ndani ya bunge. Mwishoni mwa mwezi Machi na mwanzoni mwa Aprili 2018, polisi waliwakamata viongozi tisa wa juu wa CHADEMA na kuwashtaki kwa mkusanyiko haramu na kukaidi amri ya kutawanyika baada ya kuandamana na wafuasi ili kudai utoaji wa vyeti kwa mawakala wa vituo vya kupigia kura mnamo mkesha wa uchaguzi mdogo wa Februari 2018. Kati ya wale waliokamatwa, mwenyekiti wa CHADEMA Freeman Mbowe alikabiliwa na mashtaka ya ziada, ukiwemo uchochezi. Viongozi wa CHADEMA walihusika na mapambano ya kisheria yaliyoendelea kwa muda mrefu na uamuzi bado ulikuwa ukisubiriwa.

Sheria ya uchaguzi inataja malipo ya "kiinua mgongo" ya TZS milioni 235 hadi TZS milioni 280 ($103,000 to $123,000) kwa wabunge wanaomaliza kipindi cha miaka mitano. Wabunge walio madarakani wanaweza kuzitumia fedha hizo katika kampeni za kuchaguliwa tena. NGOs na vyama vya upinzani kadhaa vilikosoa sheria hiyo kuwa inazuia wagombea ubunge wa vyama vya upinzani kutoa changamoto yenye ufanisi.

Serikali ya bara iliwaruhusu wapinzani wa kisiasa kutumia vyombo vya habari vya umma bila ya kizuizi, lakini chama tawala kilikuwa na fedha nyingi zaidi za kununua muda wa matangazo.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilikuwa ikipitia orodha ya wapiga kura ikiwa ni matayarisho ya uchaguzi mkuu wa 2020. Sheria inataka kwamba uandikishaji wapiga kura ufanyike mara mbili kila miaka mitano. Marekebesho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, hata hivyo, yalizuia uwezo wa vyama vya siasa kutoa elimu ya kiraia na kuelezea kuhusu uandikishaji wapiga kura na haki ya kupiga kura, kama walivyofanya katika siku zilizopita. Badala yake, CSOs 24 zilipewa ruhusa ya

kuendesha elimu ya kiraia. Hakuna hata mojawapo ya CSO (ambayo ilipewa ruhusa hiyo ilikuwa na fedha au uwezo wa kiufundi kufanya kampeni ya kitaifa kuhusu elimu kwa mpiga kura. Kwa kuongezea NEC ilitenga siku saba tu kwa uandikishaji katika kila mkoa, muda ambao wadau walielezea haukuwa wa kutosha kuhakikisha kuwa orodha sahihi ya wapiga kura itapatikana kabla ya uchaguzi wa 2020.

Kushiriki kwa Wanawake na Makundi ya Walio Wachache: Hakuna sheria inayoweka kiwango cha ushiriki wa wanawake au wanachama wa walio wachache katika mchakato wa kisiasa, na walishiriki. Baadhi ya watazamaji waliamini kuwa vikwazo vya kitamaduni na kifedha vilizuia ushiriki wa wanawake katika siasa. Katika uchaguzi wa mwaka 2015, wapiga kura walimchagua mwanamke kama makamu wa rais. Kulikuwa na viti maalum kwa wanawake kote katika bunge na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, ambavyo, kwa mujibu wa data za Benki ya Dunia, vilifanya jumla ya uwakilishi wa wanawake kufikia asilimia 36.

## Sehemu 4. Rushwa na Ukosefu wa Uwazi katika Serikali

Sheria inataja adhabu za jinai kwa viongozi wanaokula rushwa, lakini serikali haikutekeleza sheria hiyo ipasavyo. Mara nyingi viongozi walijihusisha na vitendo vya rushwa bila ya hofu ya kuadhibiwa. Baada ya kushika madaraka Rais Magufuli alichukua hatua kadhaa kabambe kuashiria nia yake ya dhati kupambana na rushwa. Hatua hizo zilijumuisha ukaguzi wa kushtukiza wa wizara, hospitali, na bandari ya Dar es Salaam, mara nyingi zikifuatiwa na kufukuzwa kazi mara moja kwa maafisa. Katika kutekeleza Awamu ya III (2017 - 22) ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji, Rais Magufuli alianzisha Kitengo cha Mahakama Kuu kwa ajili ya Uhujumu Uchumi, Rushwa na Uhalifu wa Kupanga mnamo mwaka 2016. Wakosoaji na waangalizi walieleza kwamba Rais Magufuli alitumia kigezo cha kupambana na rushwa ili kuwalenga wale waliokuwa wakimpinga.

Rushwa: Ingawa juhudi zilifanywa kudhibiti rushwa, bado iliendelea kuenea; hata hivyo, orodha ya Transparency International kuhusu Kiashiria cha Utambuzi wa

Rushwa iliyotolewa Februari ilionyesha maendeleo katika utambuzi wa rushwa. TAKUKURU iliripoti kwamba uchunguzi mwingi wa rushwa ulihusu serikali kuhusika katika uchimbaji wa madini, masuala ya ardhi, nishati na uwekezaji.

Matokeo ya Afrobarometer yaliyochapishwa Julai yaliashiria kwamba ufahamu wa raia kwa ujumla kuhusu rushwa ulishuka, huku asilimia 10 tu ya raia ikiripoti kwamba rushwa imeongezeka mnamo mwaka mmoja uliopita, na asilimia 71 ya raia wakihisi kwamba serikali inafanya kazi nzuri ya kupambana na rushwa. Vyombo vya serikali bado vilichukuliwa kuwa vyombo vyenye rushwa iliyokithiri, vikiongozwa na polisi, majaji na mahakimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na serikali za mitaa. NGOs ziliendelea kuripoti madai ya rushwa yaliyohusisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, maafisa wa serikali za mitaa, polisi, mamlaka za kutoa leseni, wafanyakazi wa hospitali na vyombo vya habari.

Rushwa ilitawala katika makala za magazeti, malalamiko ya raia, na ripoti za rushwa ya polisi kutoka TAKUKURU na kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mamlaka ya TAKUKURU haijumuishi Zanzibar. Mwezi Julai Mamlaka ya Zanzibar Dhidi ya Rushwa na Uhalifu wa Uchumi iliripoti kuwa iliweza kupunguza rushwa, na kutaja kesi moja ya kupatikana na hatia, na uchunguzi ambao haujakamilika kuhusu kesi za rushwa katika Wizara ya Fedha.

Kutoa Taarifa za Kifedha: Mawaziri wa serikali na wabunge, pamoja na baadhi ya watumishi wengine wa serikali, wanatakiwa kutoa taarifa za mali zao mara wanapoingia madarakani, kila mwisho wa mwaka, na wakati wanapoondoka madarakani. Sekretarieti ya Maadili hugawa fomu kila mwezi Oktoba ili zikusanywe mwezi Desemba. Kufikia mwaka 2017 asilimia 98 ya viongozi wa serikali walikuwa wamewasilisha fomu zao kwa sekretarieti (16,064 kati ya 16,339). Wakati Tundu Lissu, mbunge wa zamani wa CHADEMA, alipoondolewa kwenye kiti chake mwezi Juni, mojawapo ya sababu zilizotajwa ni kwamba hakuwasilisha fomu kuelezea kuhusu taarifa zake za kifedha. Rais aliwasilisha fomu zake na aliwasihi viongozi wengine kufanya hivyo. Ingawa adhabu zipo kwa wasiofuata amri, hakukuwa na utaratibu wa utekelezaji au njia za kutosha kuamua

usahihi wa ufichuzi wa taarifa hizo. Habari kuhusu utiifu zillichukuliwa kuwa nyeti na kupatikana tu kwa kutoa maombi kwa kamishna wa sekretarieti. Hapo awali maafisa wa sekretarieti walieleza kwamba watu ambao walishindwa kutoa taarifa walitakiwa kuonyesha sababu ya ucheleweshaji. Fomu zozote za kutangaza mali zilizowasilishwa au kukabidhiwa baada ya muda wa mwisho lazima zieleze sababu za kushindwa kufuata sheria. Taarifa za ufichuzi wa mali haziwekwi hadharani.

## Sehemu 5. Mtazamo wa Serikali Juu ya Uchunguzi wa Kimataifa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali Kuhusu Tuhuma za Ukiukaji wa Haki za Binadamu

Makundi mbalimbali ya haki za binadamu ya kitaifa na kimataifa kwa ujumla yalifanya uchunguzi na kuchapisha matokeo yao ya kesi za haki za biandamu bila kizuizi kutoka kwa serikali. Kwa ujumla mazingira ya NGOs hata hivyo yalibadilika mnamo miaka michache iliyopita. Baadhi ya NGOs za kutetea haki za binadamu zililalamika juu ya mwitikio hasi wa serikali wakati NGOs hizo zilipokosoa utendaji kazi au sera za serikali. NGOs nyingi zina wasiwasi kwamba serikali inatumia sheria ya usajili wa NGO iliyopitshwa mwezi Juni kuzifuta NGOs ambazo zinashughulika na haki za binadamu. Mwezi Agosti msajili wa NGOs alizifuta NGOs 158 kwa tabia "isiyokubaliwa," akidai kwamba NGOs hizo zilitumiwa kwa ajili ya faida na kuwanufaisha wanachama wake, mambo ambayo yako nje ya shughuli zilizoruhusiwa kwa NGO.

Mwezi Mei Msajili wa Vyama vya Kijamii katika Wizara ya Mambo ya Ndani alitoa notisi ya umma akiomba taasisi zote za kidini na mashirika ya kijamii yaliyosajiliwa chini ya wizara hiyo kuthibitisha hadhi ya usajili wao kwa nyaraka zote zilizohitajika. Mchakato huo wa nchi nzima ulianzia Dar es Salaam na mikoa ya pwani mwezi Mei na kuendelea mpaka mwisho wa mwaka huo. Kuna wasiwasi sawa kuhusu jinsi serikali inavyoweza kutumia mchakato huo kufuta mashirika ambayo yanatoa kauli zozote kuhusiana na haki za binadamu.

Umoja wa Mataifa au Taasisi Nyingine za Kimataifa: Serikali kwa ujumla ilitoa ushirikiano kwa ziara kutoka kwa wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, kama vile waandishi maalum, pamoja na wale kutoka katika mashirika maalum ya UM kama vile Shirika la Kimataifa la Kazi au taasisi nyingine za kimataifa (lakini haijumuishi NGOs) ambazo zinafuatilia haki za binadamu.

Vyombo vya Serikali vya Haki za Binadamu: Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria, na Utawala wa Umma ya muungano ina wajibu wa kuripoti na kutoa mapendekezo kuhusu haki za binadamu.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) ilitenda kazi zake bara na Zanzibar, lakini viwango vya chini vya fedha na ukosefu wa uongozi vilipunguza ufanisi wake. Tume hiyo haina mamlaka ya kisheria kuendesha mashtaka lakini inaweza kutoa mapendekezo kwa ofisi nyingine kuhusu masuluhisho au kuviarifu vyombo vya habari kuhusu ukandamizaji wa haki za binadamu na ukiukwaji na malalamiko mengine ya wananchi. Pia ina mamlaka ya kutoa maagizo ya muda mfupi kuzuia vitendo ili kuhifadhi hali ilivyo huku uchunguzi ukisuburiwa. CHRAGG pia ilitoa taarifa na ilifanya kampeni za ufahamu wa umma kuhusu masuala kadhaa. Masuala hayo yalijumuisha haja ya wakuu wa mikoa na wilaya kufuata taratibu sahihi wakati wa kutumia mamlaka yao ya kukamata, haja ya mamlaka za reli na barabara kufuata sheria na kanuni wanapofukuza wananchi kutoka kwa makazi yao, na kuvitaka vyombo vya usalama kuchunguza madai ya kutoweka au utekaji nyara, ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari, viongozi wa siasa, na wasanii.

Mnamo Septemba 19, Rais Magufuli alimteua mwenyekiti wa CHRAGG na makamishna watano.

## Sehemu 6. Ubaguzi, Dhuluma za Kijamii, na Biashara Haramu ya Kusafirisha Watu

### Wanawake

# TANZANIA

Ubakaji na Ukatili wa Majumbani: Sheria inaeleza kifungo cha maisha kwa watu ambao wamekutwa na hatia ya kubaka, ukiwemo ubakaji kwa wanandoa mnamo kipindi cha kutengana kisheria. Sheria inasema mwanamke anayetaka kuripoti ubakaji lazima afanye hivyo katika kituo cha polisi, ambako lazima apewe fomu maalum kabla ya kutafuta msaada wa matibabu. Mchakato huo ulichangia matatizo ya kiafya, kutokamilika kwa ushahidi wa kimahakama, na kushindwa kuripoti ubakaji. Mara nyingi waathiriwa walihofia kwamba kesi zilizoripotiwa kwa polisi huenda zikawekwa hadharani.

Mnamo Mei 21, Mbunge Zitto Kabwe aliikosoa serikali kushindwa kuwakamata watuhumiwa wa ubakaji katika mkoa wa Kigoma. Alirejea utaratibu unaojulikana kama teleza, wakati ambapo wakosaji wanajipaka mafuta machafu kote kwenye miili yao na kuteleza hivyo kufanya iwe vigumu kuwakamata. Kabwe alipokea ripoti ya wanawake watatu waliobakwa katika jimbo lake la uchaguzi na ambao walikuwa wamelazwa katika Hospitali ya Kigoma. NGO Tamasha ilikuwa ya kwanza kufichua kesi hizo na iliripoti jumla ya kesi 43 za ubakaji. Tamasha baadaye ilijihusisha na NGOs za haki za binadamu kama LHRC, THRDC, na Twaweza, ambazo kwa pamoja ziliibua suala hilo kwa njia ya barua kwa serikali.

Sheria inakataza mashambulio ya nguvu lakini haikatazi waziwazi ukatili wa majumbani. Ukatili wa majumbani dhidi ya wanawake uliendelea kuenea, na kwa kawaida polisi hawakuchunguza kesi kama hizo. Ripoti ya Haki za Binadamu ya Katikati ya Mwaka ya LHRC iliyohusisha kipindi cha Januari mpaka Juni ilielezea kwamba ukatili wa kingono dhidi ya watoto bado ulikuwa suala la kutia wasiwasi. LHRC, hata hivyo, haikuweza kupata data kuhusu kesi zilizoripotiwa za ukatili dhidi ya watoto wa bara. Utafiti wa vyombo vya habari na NGOs zilizofuatilia haki za binadamu ulionyesha kwamba watoto wengi waliendelea kukumbwa na ukatili wa kingono, hasa ubakaji. Kwa mujibu wa ripoti ya LHRC, asilimia 66 ya matukio makubwa ya ukatili dhidi ya watoto yalikuwa ukatili wa kingono, ambapo asilimia 90 yalikuwa ubakaji: asilimia 30 ya matukio kama hayo yaliripotiwa katika Kanda ya Ziwa (Mikoa ya Geita, Mwanza, Shinyanga, Mara, Simiyu na Kagera), huku Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ikiwa na asilimia 32.

**TANZANIA**

Kwa kawaida mamlaka hazikuwashtaki watu ambao waliwadhulumu wanawake. Watu wa karibu na waathiriwa, kama vile jamaa na marafiki, walikuwa mara nyingi ndio wakosaji. Wengi ambao walifikishwa mahakamani waliachiliwa huru kwa sababu ya rushwa katika mfumo wa mahakama, ukosefu wa ushahidi, uchunguzi duni, na hifadhi duni ya ushahidi.

Serikali ilifanya jitihada fulani kupambana na ukatili dhidi ya wanawake. Polisi walidumisha vitengo 417 vya jinsia na watoto katika mikoa yote ya nchi ili kuwasaidia waathiriwa na kushughulikia uhalifu husika. Huko Zanzibar, kwenye One Stop Centers za Unguja na Pemba, waathiriwa wangepokea huduma za afya, ushauri nasaha, msaada wa kisheria, na rufaa kwa polisi. Mwezi Agosti, Polisi wa Mkoa wa Kagera waliripoti kwamba walikuwa wameandikisha kesi 88 za ukatili wa kijinsia, kati ya Januari na Julai ambazo bado zinasubiri uamuzi mahakamani. Kesi hizo zilijumuisha kesi 46 za ubakaji, wakati nyingine zilizobaki zillihusiana na mimba katika shule.

Ukeketaji: Sheria inakataza ukeketaji kufanyiwa wasichana chini ya umri wa miaka 18, lakini haitoi ulinzi kwa wanawake wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Kwa habari kuhusu matukio ya FGM/C, angalia Kiambatisho C.

Mashtaka yalikuwa nadra. Maafisa wengi wa polisi na jamii hawakufahamu sheria, waathiriwa mara nyingi walisita kutoa ushahidi, na baadhi ya mashahidi walihofia kulipiziwa kisasi kutoka kwa wafuasi wa ukeketaji. Baadhi ya wanavijiji waliripotiwa kutoa rushwa kwa viongozi wa maeneo kutotekeleza sheria ili kuwafanyia ukeketaji mabinti zao. Wizara ya Afya iliripoti kwamba takriban asilimia 10 ya wanawake walikuwa wamepitia ukeketaji. Maeneo yenye viwango vilivyo vya juu vya ukeketaji yalikuwa Manyara (asilimia 58), Dodoma (asilimia 47), Arusha (asilimia 41), Mara (asilimia 32), na Singida (asilimia 31).

Unyanyasaji wa Kijinsia: Sheria inakataza unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake katika sehemu za kazi. Kulikuwa na ripoti kwamba wanawake waliombwa rushwa ya ngono ili kupandishwa vyeo au kupata ajira. Kwa mujibu wa Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Wanawake, kwa kawaida polisi hawakuchunguza kesi hizo. Kesi

zilizochunguzwa mara nyingi zilitupiliwa mbali kabla ya kufikishwa mahakamani --katika baadhi ya matukio hatua hiyo ilichukuliwa na walalamikaji kutokana na shinikizo la kijamii na katika matukio mengine hatua hiyo ilichukuliwa na waendesha mashtaka kutokana na ukosefu wa ushahidi. Kulikuwa na ripoti za wanawake kunyanyaswa kingono walipokuwa wakifanya kampeni kuwania uongozi, na mbunge mwanamke mmoja alisema kwamba wabunge wanawake walikumbwa na manyanyaso ya kijinsia mara kwa mara. LHRC ilitoa ripoti mwaka 2018 ikielezea kwamba wanafunzi wa kike mara kwa mara walinyanyaswa kingono katika taasisi za juu za masomo, jambo lililokaririwa na profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Tweet akimtaka Rais Magufuli kuingilia kati kwa sababu kulikuwa na matukio mengi mno ya manyanyaso katika kampasi.

Kulazimisha katika Udhibiti wa Idadi ya Watu: Hakukuwa na ripoti za utoaji mimba wa kulazimishwa au kufunga uzazi bila hiari.

Ubaguzi: Sheria inatoa hadhi sawa ya kisheria kwa wanawake na wanaume, ikiwa ni pamoja na mambo kama vile ajira, makazi, au upatikanaji wa elimu na huduma za afya; hata hivyo, sheria pia inatambua desturi za kimila ambazo mara nyingi ziliwapendelea wanaume.

Ingawa wanawake walikabiliwa na vitendo vya kibaguzi katika maeneo ya ndoa, talaka, urithi, na uraia, ubaguzi wa wazi katika maeneo kama vile elimu, mikopo, umiliki wa biashara, na makazi haukuwa wa kawaida. Hata hivyo, wanawake, hasa katika maeneo ya vijijini, walikabiliwa na changamoto kubwa sana kutokana na sababu za kitamaduni, kihistoria, na kielimu. Kwa mujibu wa ripoti ya Pengo la Kijinsia Ulimwenguni iliyotolewa na Baraza la Uchumi la Dunia mwaka 2018, wanaume wanalipwa asilimia 39 kuliko wanawake.

## Watoto

Usajili wa Kuzaliwa: Uraia unatokana na kuzaliwa ndani ya nchi au nje ya nchi kama angalau mzazi mmoja ni raia. Usajili mnamo miezi mitatu tangu kuzaliwa ni bure; wazazi wanaosubiri hadi baadaye lazima walipe ada. Huduma za umma

hazikusitishwa kwa watoto ambao hawakusajiliwa. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, kwa kushirikiana na kampuni ya mawasiliano ya Tigo, walifanikisha usajili wa kuzaliwa kwa zaidi ya watoto milioni 3.5 wenye umri wa chini ya miaka mitano ndani ya kipindi cha miaka sita iliyopita katika mikoa 13. Kwa habari za ziada, angalia Kiambatisho C.

Elimu: Elimu bure ya msingi ni ya lazima na ya watoto wote wa bara na Zanzibar mpaka wafikie umri wa miaka 15. Masomo ya shule za sekondari ni bure lakini si lazima.

Wasichana waliwakilisha takriban nusu ya watoto wote walioandikishwa katika shule za msingi lakini walikosa kwenda shuleni mara nyingi kuliko wavulana kutokana na wajibu wa nyumbani na ukosefu wa vifaa vya usafi. Katika kiwango cha sekondari, ndoa za utotoni na mimba mara nyingi vilisababisha wasichana kufukuzwa au vinginevyo kuwazuia wasichana wasimalize shule.

Chini ya Sera ya Elimu na Mafunzo iliyoanzishwa na serikali mwaka 2015, wasichana wenye mimba huenda wakarejeshwa shuleni. Mwaka 2017, hata hivyo, Rais Magufuli alitangaza kwamba wasichana hawataruhusiwa kurudi shuleni baada ya kujifungua. NGOs za haki za binadamu ziliikosoa sera hiyo kuwa ya kinyume cha katiba na sheria za nchi. Sera hiyo ilipelekea wasichana kulaumiwa na kutengwa kutoka kwa fursa za elimu, huku baba wa watoto ambao mara nyingi wakiwa walimu wao au wanaume wengine watu wazima ambao mara kwa mara hawakukabiliwa na madhara yoyote.

Dhuluma dhidi ya Watoto: Ukatili na dhuluma nyingine dhidi ya watoto zilikuwa matatizo makubwa. Adhabu ya viboko ilitumiwa shuleni, na sheria inaruhusu walimu wakuu kuwachapa wanafunzi. Utafiti wa Kitaifa wa Ukatili dhidi ya Watoto, uliofanywa mwaka 2009 (takwimu za hivi karibuni kabisa), uligundua kwamba karibu asilimia 75 ya watoto walikabiliwa na ukatili wa kimwili kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Mwezi Aprili Mahakama ya Maswa Mkoani Simiyu ilimhukumu mwalimu kifungo cha miaka 30 gerezani alipokutwa na hatia ya kubaka wanafunzi wawili wa zamani.

Mnamo Oktoba 3, sehemu za video zilionekana katika mtandao wa kijamii zikionyesha mkuu wa mkoa wa Songwe akichapa kundi la wavulana wanafunzi wa shule ya sekondari kinyume na taratibu zilizowekwa. Siku iliyofuata, Rais Magufuli hadharani aliwasihi wazazi na walimu kufanya hivyo pia.

Ndoa za Mapema na za Kulazimishwa: Sheria imeweka umri wa kisheria wa ndoa kuwa miaka 18. Marekebisho ya mwaka 2016 ya Sheria ya Mtoto yanaharamisha kuoa mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari. Ili kuzikwepa sheria hizo, iliripotiwa kwamba watu binafsi waliwahonga polisi au walilipa mahari kwa familia ya msichana kuepuka kushtakiwa. Kwa mujibu wa Human Rights Watch, wasichana wadogo wenye umri wa hata miaka saba waliozeshwa. Zanzibar ina sheria yake ya ndoa, lakini sheria hiyo haizungumzii hususan suala la ndoa za mapema. Serikali iliwezesha kampeni za kiwango cha shule za sekondari kufanyika kuhusu ukatili wa kijinsia, ambapo, katika tukio moja lililoripotiwa mwaka 2018, zilipelekea msichana mmoja kutumia maarifa hayo kuepuka ndoa ya kulazimishwa. Kwa maelezo ya ziada, angalia Kiambanisho C.

Mnamo Oktoba 23, Mahakama ya Rufaa ilikataa rufaa ya serikali kubakiza vipengele katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambavyo vingeruhusu wasichana wadogo hata wa miaka 14 kuolewa kwa idhini ya mzazi, ikiamua kwamba sheria hiyo ilikuwa kinyume cha katiba na iliwabagua wasichana. Serikali lazima sasa iondoe kipengele maalum cha ridhaa ya mzazi kwa ndoa kabla ya kufikia umri wa miaka 18.

Unyonyaji wa Watoto Kingono: Sheria inaharamisha biashara ya ngono kwa watoto na ponografia ya watoto. Watu wanaopatikana na hatia ya kuwezesha ponografia ya watoto wanakabiliwa na faini ya kuanzia TZS milioni moja ($440) hadi TZS milioni 500 ($220,000), kifungo cha mwaka mmoja hadi miaka 20 gerezani, au vyote viwili. Wale wanaopatikana na hatia ya biashara ya ngono ya watoto wanakabiliwa na faini ya kuanzia TZS milioni tano ($2,200) hadi TZS milioni 150 ($66,000), kifungo cha miaka 10 mpaka 20, au vyote viwili. Hakukuwa na mashtaka yoyote kutokana na sheria hiyo mnamo mwaka huo.

Sheria inataja kwamba kufanya ngono na mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18 ni ubakaji isipokuwa ndani ya ndoa ya kisheria. Sheria hiyo haikutekelezwa kila mara kwa sababu ya visa kutoripotiwa au kwa sababu wasichana waliokabiliwa na shinikizo walifuta mashtaka. Kwa mfano kulikuwa na visa vya ubakaji wa wasichana ambavyo havikuripotiwa Zanzibar.

Mauaji ya Watoto Wachanga au Watoto wenye Ulemavu: Mauaji ya watoto wachanga yaliendelea, hasa miongoni mwa akina mama maskini wa vijijini ambao waliamini wao wenyewe hawakuweza kumudu kulea mtoto. Takwimu za kitaifa hazikupatikana.

Watoto wasio na Makazi: Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, idadi kubwa ya watoto walikuwa wakiishi na kufanya kazi barabarani, hasa katika miji na karibu na mipaka. Wizara hiyo iliripoti kwamba watoto 6,132 walikuwa wakiishi katika mazingira hatari mnamo mwaka huo. Watoto hao walikuwa na nafasi ndogo ya kupata huduma za afya na elimu, kwa sababu hawakuwa na makazi ya kudumu au pesa za kununua dawa, sare za shule, na vitabu. Wao pia walikuwa katika hatari ya kukabiliwa na dhuluma za kingono.  Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto, kuanzia Julai 2018 mpaka Machi, watoto 13,420 wasiokuwa na makazi walipewa mahitaji yakiwemo chakula, nguo, elimu, na afya kutoka kwa serikali pamoja na taasisi binafsi.

Utekaji Nyara wa Watoto Kimataifa: Tanzania si mwanachama wa Mkataba wa Hague wa mwaka 1980 kuhusu Vipengele vya Kiraia vya Utekaji Nyara wa Watoto Kimataifa. Tazama Ripoti ya Kila Mwaka ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani kuhusu Utekaji Nyara wa Watoto Unaofanywa na Wazazi Kimataifa kwenye https://travel.state.gov/content/travel/en/International-Parental-Child-Abduction/for-providers/legal-reports-and-data.html.

**Chuki Dhidi ya Wayahudi**

Idadi ya Wayahudi ni ndogo sana, na hakukuwa na ripoti za vitendo vya chuki dhidi ya Wayahudi.

## Biashara Haramu ya Kusafirisha Watu

Tazama Ripoti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya Biashara Haramu ya Kusafirisha Watu kwenye https://www.state.gov/trafficking-in-person-report/.

## Watu Wenye Ulemavu

Sheria inakataza ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu wa kimwili, hisia, taaluma na akili, lakini serikali haikuimarisha vipengele hivyo kwa ufanisi.

Majengo machache ya umma yaliweza kufikiwa na watu wenye ulemavu. Majengo mapya ya umma, hata hivyo, yalijengwa kulingana na sheria. Sheria inatoa masharti ya upatikanaji wa habari na mawasiliano, lakini baadhi ya watu wenye ulemavu hawakuwa na upatikanaji huo.

Kulikuwa na wanachama sita wa bunge la muungano wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu walishikilia viti vitatu maalum katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Ofisi ya Waziri Mkuu inajumuisha nafasi ya waziri inayoshughulikia ulemavu. Nchi inafafanua watu wenye ualbino kama walemavu na ilimteua mtu mwenye ualbino kuwa balozi wa nchi huko Ujerumani mwaka 2017.

Vikomo vya ushiriki wa kisiasa kwa watu wenye ulemavu vilijumuisha vituo vya kupigia kura ambavyo havikuweza kufikika, ukosefu wa upatikanaji wa taarifa, ujumuisho mdogo katika vyama vya siasa, kushindwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutekeleza maelekezo kuhusu ulemavu, na chuki bila ya sababu dhidi ya watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2008 wa Watu wenye Ulemavu Tanzania, ilikadiriwa asilimia 53 ya watoto wenye ulemavu walihudhuria shule. Hakukuwa

na violezo muhimu vilivyoripotiwa kuhusu dhuluma katika vifaa vya elimu au vya afya ya akili.

**Vitendo vya Ukatili, Ubaguzi na Dhuluma Nyingine Kutokana na Mwelekeo wa Jinsia na Utambulisho wa Kijinsia.**

Tabia ya kukubaliana kujamiana kwa jinsia ya aina moja ni kinyume cha sheria nchini. Sheria ya bara na Zanzibar huadhibu "mwenendo mchafu" kwa kifungo cha hadi miaka mitano gerezani au faini. Sheria humwadhibu mtu yeyote ambaye anapatikana na hatia ya kufanya "ngono na mtu mwingine kinyume cha maumbile au anamruhusu mwanamme kufanya naye ngono kinyume cha maumbile" kwa kifungo cha miaka 30 hadi maisha upande wa bara na kifungo cha hadi miaka 14 Zanzibar. Visiwani Zanzibar, sheria pia inatoa masharti ya kifungo cha hadi miaka mitano gerezani au faini kwa "vitendo vya usagaji." Zamani mahakama ziliwashtaki kwa uzururaji au ukahaba watu waliotuhumiwa kwa tabia za ngono kwa watu wa jinsia moja. Sheria haikatazi ubaguzi kwa misingi ya mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia. Mara nyingi polisi waliwanyanyasa watu walioaminiwa kuwa LGBTI kutokana na mavazi yao au tabia zao.

Mnamo mwaka huo serikali ilipinga ulinzi bora wa haki za watu wa LGBTI, ambao ilibainisha kuwa ni kinyume cha sheria ya nchi na kanuni za utamaduni wa jamii. Viongozi waandamizi wa serikali walitoa kauli kadhaa dhidi ya LGBTI. Mnamo Septemba 20, naibu waziri wa mambo ya ndani aliwaamuru polisi wa Zanzibar kuwakamata wanachama wa jumuiya za LGBTI, akiwashutumu kwa kukosa maadili, kutokubaliwa, na haramu, na kuleta taswira mbaya visiwani na kuhusishwa na matumizi ya madawa ya kulevya. Mnamo mwaka huo kulikuwa na ripoti moja kwamba polisi waliwakamata washukiwa wawili kwa shutuma za kujihusisha na vitendo vya ushoga na kuwalazimisha wafanyiwe vipimo vya njia ya haja kubwa. Pia kulikuwa na ripoti za kukamatwa na kuwekwa kizuizini ili kuwanyanyasa wanaharakati waliojulikana wa LGBTI.

Watu wa LGBTI waliendelea kuogopa kuripoti ukatili na uhalifu mwingine, ukiwemo ule uliofanywa na mawakala wa serikali, kutokana na hofu ya

kukamatwa. Watu wa LGBTI walikabiliwa na ubaguzi wa kijamii uliowazuia wasipate huduma za afya, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa habari kuhusu VVU, makazi, na ajira. Hakukuwa na juhudi za serikali zilizojulikana za kupambana na ubaguzi kama huo.

Mwezi Januari, baada ya kukamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja, watu 17 waliripotiwa kufanyiwa vipimo vya lazima vya njia ya haja kubwa katika Hospitali ya Serikali ya Kigongoni, Arusha, na wafanyakazi wa afya mbele ya polisi wenye silaha. Waathiriwa hawakuwa na wakili au mwakilishi yeyote, na "matokeo" hayajawahi kutolewa.

Mwaka 2017 mamlaka ziliwasilisha kesi dhidi ya wanawake wawili huko Mwanza ambao walirekodiwa kwenye video iliyosambazwa katika mitandao ya kijamii wakivishana pete katika sherehe ya uchumba. Kesi hiyo ilifutwa bila ya kusikilizwa mwaka 2018 halafu ikafunguliwa tena kama kesi mpya mwezi Juni.

Mwezi Aprili mwanafunzi mwenye umri wa miaka 19 katika Seminari ya Kiislamu ya Katoro alifariki baada ya kupigwa na mwalimu na wanafunzi wenzake. Iliripotiwa walimpiga kwa sababu alidaiwa kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja. Alizikwa bila ya familia yake kujulishwa; waliwasiliana na polisi walipogundua mtoto wao hajulikani alipo. Baada ya uchunguzi, polisi waliwakamata walimu wanne na wanafunzi 11. Polisi pia walipata amri ya mahakama kufukua mabaki ya mwili kwa uchunguzi zaidi.

**Unyanyapaa wa Kijamii kwa VVU na UKIMWI**

Ripoti ya Vielelezo ya mwaka 2013 ya Watu Wanaoishi na Unyanyapaa wa VVU ilionyesha kwamba watu wenye VVU/UKIMWI walipitia viwango vikubwa vya unyanyapaa nchini kote (asilimia 39), huku unyanyapaa ukiwa hasa wa juu jijini Dar es Salaam (asilimia 50). Aina za kawaida za unyanyapaa na ubaguzi walizokabiliana nazo zilikuwa umbeya, matusi, na kutojumuishwa katika shughuli za kijamii, kifamilia, na kidini. Zaidi ya mtu mmoja kati ya watu watano wenye VVU/UKIMWI walipitia mabadiliko ya kulazimishwa ya makazi au kushindwa

kukodi mahali pa kukaa. Jijini Dar es Salaam, takriban mtu mmoja kati ya watu watatu kama hao amewahi kupoteza kazi au chanzo kingine cha mapato.

Sheria inakataza ubaguzi dhidi ya mtu yeyote "anayejulikana au kutambuliwa" kuwa na VVU na inaweka viwango vya tiba kwa usiri ili kuwalinda watu wenye VVU/UKIMWI. Dhuluma za polisi dhidi ya watu wenye VVU, hasa miongoni mwa makundi matatu muhimu ya watu (wanaofanya biashara ya ngono, watumiaji wa dawa za kulevya, na watu wa LGBTI) zilijumuisha kukamatwa kiholela, unyang'anyi, na kukataa kupokea malalamiko kutoka kwa waathiriwa wa uhalifu. Katika sekta ya afya, makundi muhimu ya watu yalipata adha ya kunyimwa huduma, unyanyasaji wa maneno, dhuluma, na ukiukwaji wa usiri. Mwaka 2017 serikali iliruhusu huduma za kijamii kwa makundi muhimu ya watu kurejeshwa mahali pake baada ya kutolewa miongozo iliyosahihishwa, ingawa usambazaji wa mafuta ya kulainisha bado yamepigwa marufuku. NGOs na CSOs zinazohudumia makundi hayo muhimu ya watu ziliendelea kukabiliana na upinzani na unyanyasaji wa mara kwa mara kutoka kwa watekelezaji wa sheria. Kulikuwa na hofu iliyoendelea miongoni mwa NGOs hizo kufanya kazi kwa uhuru na kwa uwazi, pamoja na miongoni mwa watu wa LGBTI kutafuta huduma za afya kwa uhuru, ikiwa ni pamoja na uzuiaji wa matibabu ya VVU.

Madawati ya jinsia katika vituo vya polisi nchini kote yalianzishwa ili kusaidia kushughulikia hali ya kutoaminiana kati ya wanachama wa makundi maalum ya watu na polisi.

**Ukatili au Ubaguzi Mwingine wa Kijamii**

Licha ya jitihada za serikali na NGOs ili kupunguza ukatili wa makundi kupitia kwa elimu ya wananchi na polisi jamii, ukatili wa makundi uliendelea kutokea. Kwa mujibu wa ripoti ya LHRC ya katikati ya mwaka, watu 385 waliuawa katika ghasia za makundi. Kwa mfano, mwezi Juni, katika mji wa Shinyanga, Esther Samwel aliuawa na kundi la watu wenye hasira baada ya kushutumiwa kuiba mboga sokoni.

## TANZANIA

Mauaji yanayohusiana na uchawi yaliendelea kuwa tatizo. Kwa mujibu wa ripoti ya LHRC ya katikati ya mwaka, kulikuwa na mauaji 106 yaliyohusiana na uchawi kutoka Januari mpaka Juni. Waathiriwa wakuu au walengwa wa mauaji hayo waliendelea kuwa wanawake wazee na watoto. Mikoa yenye idadi kubwa ya mauaji ilikuwa Mbeya, Iringa, Dar es Salaam, na Shinyanga. Kwa mfano, mjini Dar es Salaam, polisi walimkamata mwanamume mmoja kwa kumwuza mtoto wake wa kike wa miaka sita auawe ili viungo vyake vya mwili vitumiwe katika dawa za kumtajirisha. Mwili wa mtoto huyo uligunduliwa ukiwa umekatwa kichwa katika mkoa wa Mbeya na mguu wake wa kulia ukiwa umekatwa.

Kuanzia Januari mpaka Juni, watoto 10 katika mkoa wa Njombe waliripotiwa kutoweka na kugunduliwa baadaye wakiwa wamekufa huku baadhi ya viungo vya mwili visipokuwepo. Kuhusiana na kesi hiyo, washukiwa 28 walikamatwa.

Mnamo mwaka 2015 serikali iliwapiga marufuku wachawi katika jaribio la kutokomeza mauaji ya watu wenye ualbino. Mashambulizi kwa watu wenye ualbino yalikuwa yakishuka, na kuanzia Januari mpaka Juni, hakukuwa na ripoti ya kesi zozote za watu ambao wana ualbino kuuawa au kushambuliwa. Watu wenye ualbino walibakia kuwa katika hatari ya kufanyiwa ukatili, hata hivyo, hasa wakati wa kipindi cha uchaguzi, kwani baadhi ya watendaji wa matambiko walitafuta viungo vya mwili wa albino wakiamini kwamba vingeweza kutumiwa kuleta madaraka, utajiri, na bahati nzuri. Shule zilizotumiwa kama makazi ya muda mfupi katika baadhi ya matukio zilibadilishwa kuwa makazi ya muda mrefu, huku wanafunzi wengi wenye ualbino wakiogopa kurudi nyumbani kwao. Eneo moja la makazi la Buhangija, hata hivyo, lilikuwa na takriban watoto 470 wenye ualbino walioishi huko, lakini iliripotiwa kwamba 350 kati ya watoto hao wameungana na familia zao. Kusambaa kwa ubaguzi dhidi ya watu wenye ualbino bado ulikuwepo. Mnamo mwaka huo mwanamke mmoja mwenye ualbino aliripotiwa kunyanyaswa kazini kwake mjini Mwanza na wafanyakazi wenzake. Mwanamke huyo alipoteza kazi yake kama mhudumu katika mgahawa wa hoteli na badala yake akaambiwa afanye kazi ya kusafisha vyumba.

Wakulima na wafugaji mara nyingine waligombania maeneo ya kiasili ya malisho, na ukatili uiliendelea kuzuka wakati wa baadhi ya migogoro.

## Sehemu ya 7. Haki za Wafanyakazi

### a.Uhuru wa Kushiriki na Haki ya Mapatano ya Pamoja

Serikali za bara na Zanzibar zina sheria tofauti za kazi. Wafanyakazi wa bara, isipokuwa kwa wafanyakazi katika makundi ya "huduma ya kitaifa" na walinzi wa magereza, wana haki ya kuanzisha na kujiunga na vyama huru vya wafanyakazi, kupatana kwa pamoja, na kufanya migomo ya kisheria. Sheria inatakaza ubaguzi dhidi ya vyama vya wafanyakazi. Hata hivyo, serikali ilizuia haki hizo. Kurejeshwa kwa wafanyakazi waliofukuzwa kwa ajili ya shughuli za chama cha wafanyakazi si lazima.

Vyama vya wafanyakazi katika sekta binafsi lazima viwe na zaidi ya wanachama 20 na kujiandikisha na serikali, huku vyama vya sekta ya umma vikihitaji wanachama 30. Mashirika matano yanahitajika ili kuunda shirikisho. Ushirikiano wa chama cha wafanyakazi na mashirika yasiyo ya wafanyakazi unaweza kubatilishwa na Mahakama ya Kazi kama uliundwa bila idhini ya serikali, au kama umoja huo unachukuliwa kuwa shirika ambalo msaada wake ni mpana kuliko mahusiano ya mfanyakazi na muajiri. Chama cha wafanyakazi au chama cha waajiri lazima kiombe usajili kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi katika Wizara ya Kazi mnamo miezi sita tangu kuanzishwa. Hata hivyo, sheria haitoi muda maalum ambapo lazima serikali isajili shirika, na msajili ana uwezo wa kukataa usajili kwa misingi ya upande mmoja au yenye utata. Serikali inatoa misingi ya ofisi ya viongozi wa chama cha wafanyakazi. Kushindwa kuzingatia mahitaji ya serikali kunapelekea faini, kifungo gerezani au vyote viwili.

Sheria inavitaka vyama viwasilishe rekodi za kifedha na orodha ya wanachama kwa msajili kila mwaka na kupata idhini ya serikali ya kushirikiana na vyama vya wafanyakazi vya kimataifa. Msajili anaweza kuiomba Mahakama ya Kazi kufuta

usajili au kusimamisha vyama kama kuna kuingiliana kibiashara au kama inaamuliwa kwamba chama fulani kilikiuka sheria au kuhatarisha usalama wa raia.

Makubaliano ya mapatano ya pamoja lazima yasajiliwe na Tume ya Kazi. Watumishi wa umma, isipokuwa kwa mambo machache ya kipekee, kama vile wafanyakazi wanaohusika na "huduma ya kitaifa" na askari wa magereza, pia wanaweza kushiriki majadiliano ya pamoja.

Waajiri wana haki ya kuanzisha shughuli ya kuwafungia wafanyakazi nje ilimradi wanazingatia mahitaji na taratibu fulani za kisheria. Ili mgomo utangazwe kuwa halali, sheria inahitaji taarifa tatu tofauti za dhamira, muda wa kusubiri wa angalau siku 92, na kura ya chama inayopigwa mbele ya afisa wa Wizara ya Kazi huku ikikusanya idhini ya angalau asilimia 75 ya wanachama wanaopiga kura. Pande zote katika mgogoro zinawajibika katika makubaliano ya usuluhishi, na hakuna upande wowote utakaofanya mgomo au kufungia wafanyakazi nje mpaka mchakato huo ukamilike. Migogoro kuhusu marekebisho au masharti ya mikataba iliyosainiwa lazima yashughulikiwe kupitia kwa usuluhishi na hayawezi kuwa chanzo cha migomo.

Sheria inazuia haki ya kugoma ikiwa mgomo unaweza kuhatarisha maisha na afya ya watu. Kushawishi wengine kwa kuunga mkono mgomo au kupinga sheria ya kuzuia wafanyakazi wasiingie sehemu zao za kazi kumepigwa marufuku. Wafanyakazi katika sekta zilizofafanuliwa kuwa "muhimu" (maji na usafi wa mazingira, umeme, huduma za afya na huduma zinazohusiana na maabara, zimamoto, udhibiti wa safari za anga, mamlaka ya anga, mawasiliano ya simu, na huduma zozote za usafiri zinazohitajika kwa ajili ya utoaji wa huduma hizi) wasigome bila ya makubaliano ya awali ya kuendelea kutoa "huduma ndogo ndogo." Wafanyakazi katika sekta nyingine pia huenda wakawa katika kiwango hicho kutegema jinsi inavyoamuliwa na Kamati ya Huduma Muhimu, kamati ya pande tatu inayojumuisha waajiri, wafanyakazi na wawakilishi wa serikali wenye mamlaka ya kufanya maamuzi kila baada ya kipindi fulani kubaini zipi ni huduma muhimu.

Kulingana na Sheria ya Ajira ya Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, kisheria mwajiri hapaswi kumuachisha kazi mfanyakazi kwa kushiriki mgomo halali au kumuachisha kazi mfanyakazi anayekubali masharti ya mwajiri wakati wa mgomo.

Adhabu za ukiukwaji hazikuwa za kutosha kuzuia ukiukwaji. Migogoro juu ya misingi ya ubaguzi dhidi ya umoja wa wafanyakazi lazima ifikishwe kwa Kamishna wa Usuluhishi na Maelewano, idara ya serikali ambayo ina mahusiano na Wizara ya Kazi. Hakukuwa na taarifa za umma kuhusiana na kesi za ubaguzi dhidi ya umoja wa wafanyakazi.

Hakukuwa na ripoti za migomo ya kisekta au migomo yoyote mikubwa nchini.

Visiwani Zanzibar sheria inahitaji chama chochote chenye wanachama 50 au zaidi kisajiliwe, kiwango ambacho makampuni machache yanaweza kukidhi. Sheria inaweka viwango kwa maafisa wa vyama vya wafanyakazi kujua kusoma na kuandika. Sheria inampa msajili madaraka makubwa ya kuzuia usajili kwa kuweka vigezo vya kuamua iwapo katiba ya shirika ina vipengele vinavyofaa kulinda maslahi ya wanachama wake. Sheria hiyo inatumika kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi na inapiga marufuku wafanyakazi wa Zanzibar kujiunga na vyama vya wafanyakazi Tanzania Bara. Sheria inatakaza chama kutumia fedha zake, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kulipa faini au adhabu zozote walizopata viongozi wa chama cha wafanyakazi katika utekelezaji wa majukumu yao rasmi. Visiwani Zanzibar wafanyakazi wa serikali na wa sekta binafsi wana haki ya kugoma ilimradi wanafuata taratibu zilizoainishwa katika sheria ya kazi. Kwa mfano, wafanyakazi wa sekta muhimu wasigome; wengine lazima wawape mamlaka za usuluhishi angalau siku 30 kutatua suala la mgogoro na kutoa notisi ya mapema ya siku 14 ya hatua yoyote ya mgomo inayopendekezwa.

Sheria inaruhusu mapatano ya pamoja katika sekta binafsi. Watumishi wa umma pia wana haki ya kufanya mapatano kwa pamoja kupitia Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na wafanyakazi wa Afya; hata hivyo, wanachama wa jeshi la polisi na wa magereza, na viongozi wa ngazi za juu wa umma (kwa mfano mkuu wa shirika

la utendaji) hawaruhusiwi kujiunga na chama cha wafanyakazi. Kitengo cha Kushughulikia Migogoro Zanzibar kinashughulikia migogoro ya kazi. Visiwani Zanzibar majaji na maafisa wote wa mahakama, wanachama wa idara maalum, na wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi hawajumuishwi katika ulinzi wa sheria ya kazi.

Visiwani Zanzibar mahakama ni mahali pekee ambako migogoro ya kazi inaweza kusikilizwa. Kwa mujibu wa Tume ya Kazi Zanzibar, wafanyakazi 16 walitumia mahakama kwa ajili ya migogoro ya kazi. Utekelezaji wa kazi Zanzibar hautoshi, hasa katika kisiwa cha Pemba.

Serikali haikutekeleza kwa ufanisi sheria ya kulinda haki za mapatano ya pamoja. Kwa upande wa bara na huko Zanzibar, waajiri wa sekta binafsi walipitisha sera au mbinu dhidi ya umoja, ingawa shughuli za kibaguzi zinazofanywa na mwajiri dhidi ya wanachama wa umoja wa wafanyakazi ni haramu. Ripoti ya mwaka 2018 ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) ilidai kwamba wachimba madini wa kimataifa waliwahonga viongozi wa serikali kupuuza malalamiko ya wafanyakazi na kuandika ripoti nzuri za uongo kuhusu mazingira ya kazi katika machimbo ya madini. TUCTA pia iliripoti kwamba waajiri waliwakatisha tamaa wafanyakazi wasipatane kwa pamoja halafu wakalipiza kisasi dhidi ya wanarakati wanaotetea haki za wafanyakazi kwa njia ya kusitisha ajira zao na hatua nyingine. Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi wa Madini, Nishati, Ujenzi na Ushirika wa Wafanyakazi walikutana mwezi Juni kujadili jinsi ya kuboresha mipango katika sekta ya madini.

TUCTA pia ilielezea wasiwasi wake juu ya pendekezo la mfumo mpya wa mkokotoo wa mafao ya uzeeni. Chini ya mfumo huo mpya, asilimia 25 itatolewa kama malipo ya pamoja huku asilimia 75 iliyobaki ikilipwa kidogo kidogo kila mwezi. TUCTA iliitaka serikali irudi kwenye mfumo wa zamani, ambapo wafanyakazi walilipwa asilimia 50 ya malipo wakati wa kustaafu. Ilipofika mwisho wa Desemba 2018, Rais Magufuli alitangaza kwamba mfumo mpya hautaanza kutumika mpaka mwaka 2023 ili kutoa muda zaidi wa kufikia muafaka.

## b. Ukatazaji wa Kazi za Kulazimishwa au Kushurutishwa

Sheria inakataza aina nyingi ya kazi za kulazimisha au kushurutisha. Sheria inaruhusu wafungwa kufanya kazi bila ya malipo katika miradi ya ujenzi na kilimo ndani ya magereza. Sheria inachukulia kwamba kazi kama hiyo inakubalika ilimradi mamlaka ya umma imehakikisha kwamba kazi hiyo si kwa manufaa ya upande wowote binafsi. Sheria pia inaruhusu kazi kufanyika kama sehemu ya huduma ya lazima ya kitaifa katika mazingira maalum. Katiba imeweka wazi kwamba hakuna kazi itakayochukuliwa kuwa kazi ya kulazimishwa endapo kazi hiyo ni sehemu ya huduma ya lazima ya taifa kwa mujibu wa sheria, au "jitihada ya kitaifa ya kuhamasisha rasilimali za binadamu kwa ajili ya kuimarisha jamii na uchumi wa kitaifa na kuhakikisha maendeleo ya tija ya kitaifa."

Sheria imeweka adhabu za jinai kwa waajiri wanaotumia wafanyakazi kwa nguvu, lakini adhabu hazitoshi kuzuia ukiukwaji. Serikali haikutekeleza sheria hiyo kikamilifu. Serikali na pia Shirika la Kimataifa la Kazi (ILO) havikutoa takwimu kuhusu utendaji wa serikali. ILO iliripoti matukio ambayo hayakutajwa ya ajira za kulazimisha, zikiwemo zile ambazo zinawahusu watoto kutoka mikoa ya nyanda za juu kusini waliolazimishwa kufanya kazi za majumbani au kazi za mashambani, katika machimbo, na katika sekta isiyo rasmi ya biashara. Ajira za kulazimisha kwa mtoto zilitokea (angalia Sehemu ya 7. c). Mwishoni mwa mwaka 2018 serikali iliandika rasimu ya kitaifa ya mkakati wa ajira kwa watoto, ambayo bado haijazinduliwa rasmi.

Wafungwa walifanya kazi bila ya kulipwa na kazi zisizo za hiari kwa miradi nje ya magereza, kama vile ukarabati wa barabara, kilimo, na miradi ya ujenzi ya serikali. Wizara ya Mambo ya Ndani iliripoti kwamba wafungwa walifanya kazi kwenye mradi wa kilimo cha miwa, ikiwemo kupanda eka 2,000 za miwa chini ya mkataba kati ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF). Idara ya magereza ya Moshi, kwa kushirikiana na PPF, waliweka vifaa kwenye kiwanda cha ngozi, na wafungwa walitengeneza viatu na mikoba.

Pia tazama Ripoti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya '*Biashara Haramu ya Kusafirisha Watu* kwenye www.state.gov/traffikicing-in-person-report/.

## c. Kukataza Ajira kwa Watoto na Umri wa Chini Kuajiriwa

Sheria inakataza unyonyaji wa watoto katika sehemu za kazi. Kwa mujibu wa sheria umri wa chini wa ajira ya kibarua ni miaka 14 kwa bara; Zanzibar umri wa chini wa ajira ni miaka 15. Watoto wanaozidi umri wa miaka 14 lakini walio chini ya umri wa miaka 18 wanaweza kuajiriwa kufanya kazi nyepesi tu zisizopelekea madhara kwa afya na maendeleo yao, au mahudhurio shuleni. Serikali ilichapisha kanuni za kufafanua kazi zenye madhara kwa watoto katika sekta kadhaa, ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, uvuvi, madini, na uchimbaji mawe, ujenzi, huduma, shughuli zisizo rasmi, na usafiri. Sheria imeweka hususan ukomo wa saa za kufanya kazi kwa watoto kuwa masaa sita kwa siku. Adhabu hazikutosha kuzuia ukiukwaji, na hakukuwa na visa vya mashtaka vilivyoripotiwa chini ya sheria hiyo.

Serikali haikutekeleza sheria hiyo kwa ufanisi. Ukosefu huo wa utekelezaji uliwaacha watoto katika hatari ya unyonyaji huku wakiwa na ulinzi mdogo. Ajira kwa watoto ilikuwa imeenea katika sekta za kilimo, uchimbaji madini, viwanda, uvuvi, na kazi za majumbani. Awali ILO ilifanya kazi na serikali ili kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa kazi kuhusu ajira kwa watoto, lakini hakukuwa na shughuli kama hizo zilizoripotiwa mnamo mwaka huo.

Kesi za ajira kwa watoto zilifikishwa mahakamani bara. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake, na Watoto ya Zanzibar haikuchukua hatua za kisheria zinazohusiana na ajira kwa watoto.

Hatua za serikali kukabiliana na ajira kwa watoto zilijumuisha kuhakikisha kwamba watoto wenye umri wa kwenda shule walikwenda shule, kuweka adhabu kwa wazazi ambao hawakuwaandikisha watoto wao shule, na kuwashinikiza waajiri katika sekta rasmi wasiwaajiri watoto chini ya miaka 18. Mnamo Septemba 2018 Rais Magufuli alimteua kamishna mpya wa kazi ambaye aliripotiwa

kuorodhesha kupunguza ajira kwa watoto kama mojawapo ya vipaumbele vyake. Nchi iliendeleza mkakati wa kitaifa wa ajira kwa watoto mwaka 2018; hata hivyo, serikali bado haijauzindua mkakati huo.

Tanzania bara, watoto walifanya kazi kama wafanyakazi wa majumbani, wachuuzi wa mitaani, na wauzaji madukani na vilevile ukulima mdogo, biashara za familia, uvuvi, ujenzi, na uchimbaji mdogo wa dhahabu na tanzanite. Kwa mujibu wa Human Rights Watch, hata watoto wenye umri mdogo wa miaka minane walifanya kazi katika uchimbaji wa madini. Huko Zanzibar, kimsingi watoto walifanya kazi za uvuvi, kuchuma karafuu, kazi za majumbani, biashara ndogo ndogo, na upasuaji wa kokoto.

Visiwani Zanzibar jitihada za serikali kudhibiti ajira kwa watoto zilikuwa ndogo. Katika wilaya ya Micheweni, na vijiji vya Mwambe, kwa mfano, watoto walijihusisha na upasuaji mawe. Katika vijiji vya uvuvi kama Matemwe, watoto hawakwenda shule lakini walifanya kazi katika soko la samaki.

Pia tazama katika Wizara ya Kazi *Ugunduzi kuhusu Aina Mbaya Kabisa za Ajira kwa Watoto* kwenye www.dol.gov/agencies/ilab/resources/reports/child-labor/finding na katika Wizara ya Kazi *Orodha ya Bidhaa zilizozalishwa na Ajira kwa Watoto au Ajira za Kulazimishwa* kwenye https://www.dol.gov/agencies/ilab/reports/child-labor/list-of-goods.

**d. Ubaguzi kuhusiana na Ajira na Aina ya Kazi**

Sheria ya ajira na mahusiano kazini inakataza ubaguzi sehemu za kazi, wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, dhidi ya mfanyakazi yeyote katika misingi ya rangi, utaifa, kabila, au mahali pa asili, mbari, asili ya kitaifa, asili ya kijamii, maoni ya kisiasa au dini, jinsi, jinsia, ujauzito, hadhi ya ndoa au majukumu ya kifamilia, ulemavu, VVU/UKIMWI, umri, au hali ya maisha. Sheria haikatazi hususan ubaguzi kwa misingi ya mwelekeo wa kijinsia au utambulisho wa kijinsia, lugha, uraia, au hadhi nyingine ya ugonjwa wa kuambukiza. Sheria inatofautisha

kati ya ubaguzi na mwajiri kuajiri au kupandisha cheo mtu fulani kwa kuzingatia taratibu za sera ya upendeleo unaoshabihiana na kuendeleza usawa, au kuajiri kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kazi. Serikali kwa ujumla haikutekeleza sheria hiyo kwa ufanisi, na adhabu hazikutosha kuzuia ukiukaji.

Wanawake wana hadhi sawa na wanaume chini ya sheria ya kazi Tanzania Bara. Kwa mujibu wa TUCTA, ubaguzi wa kijinsia katika misingi ya mishahara, kupandishwa cheo, na ulinzi wa kisheria katika ajira uliendelea kutokea katika sekta binafsi. Ilikuwa vigumu kuthibitisha na mara nyingi haukuadhibiwa. Ingawa waajiri katika sekta rasmi walikuwa makini zaidi na sheria dhidi ya ubaguzi, matatizo yalikuwa makubwa hasa katika sekta isiyo rasmi, ambapo idadi ya wanawake waliajiriwa kwa kutolingana na wanaume. Mara nyingi wanawake walikuwa wakiajiriwa kwa mishahara midogo na katika ajira za hatari, na waliripoti viwango vya juu vya uonevu, vitisho, na unyanyasaji wa kijinsia. Utafiti wa mwaka 2015 uliofanywa na LHRC uligundua kwamba wanawake walikabiliwa na ubaguzi hasa katika viwanda vya uchimbaji madini, chuma, na usafiri. Ripoti ya mwaka 2017 ya LHRC juu ya haki za binadamu na biashara inaonyesha kwamba wanawake bado walikumbwa na ubaguzi.

Ubaguzi dhidi ya wafanyakazi wahamiaji ulitokea pia. Mara nyingi wao walikabiliwa na matatizo katika kutafuta ajira zenye kutambulika nje ya sekta zisizo rasmi. Sheria ya mwaka 2015 ya Udhibiti wa Ajira za Wageni inampa kamishna wa kazi mamlaka ya kukataa kutoa vibali vya kazi kama ikiwa mwananchi mwenye ujuzi sawa anapatikana. Mnamo mwaka huo watalaamu wa kigeni, ikiwa ni pamoja na maafisa waandamizi wa mashirika ya kimataifa, mara kwa mara walikabiliwa na matatizo ya kupata au kuongeza muda wa vibali vya kazi. Kwa sababu wakimbizi waliishi katika kambi na hawakuweza kusafiri kwa uhuru (tazama sehemu ya 2.d.), wachache walifanya kazi katika sekta rasmi. Ingawa jitihada za wahusika wa mashirika yasiyo ya kiserikali na wale wa serikali zilifanywa ili kuzuia ubaguzi na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, LHRC iliripoti kwamba watu wa kundi hilo walikuwa bado wakiishi kwa hofu ya usalama wao binafsi na kwa hiyo hawakuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za

kijamii, kiuchumi na kisiasa. LHRC pia ilisema kwamba watu wenye ulemavu pia walikabiliwa na ubaguzi katika kutafuta ajira na fursa ya kufika mahali pa kazi.

Ukaguzi uliofanywa tangu kupitishwa kwa sheria hiyo mwaka 2015 umebaini kuwa wafanyakazi 779 wa kigeni walifanya kazi bila ya vibali sahihi. Kati yao, 29 walirejeshwa makwao na 77 walifikishwa mahakamani. Kwa sababu wakimbizi halali waliishi katika kambi na hawakuweza kusafiri kwa uhuru (tazama Sehemu 2.d.), wachache walifanya kazi katika sekta rasmi.

**e. Mazingira ya Kazi Yanayokubalika**

Mwaka 2015 serikali iliweka kiwango cha kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa sekta za umma na binafsi kwa upande wa bara, na kuvigawa viwango hivyo katika sekta tisa za ajira. Kiwango cha chini cha mshahara kilikuwa juu ya mstari wa umaskini, lakini katika viwanda vingi, kilikuwa chini ya viwango vya Benki ya Dunia kwa kile kinachojumuisha umaskini uliokithiri. Mstari wa umaskini wa serikali haujafanyiwa marekebisho tangu mwaka 2012. Sheria iliwaruhusu waajiri kutuma maombi kwa Wizara ya Kazi kwa ajili ya msamaha wa kulipa kiwango cha chini cha mshahara. Sheria za kazi zinahusu wafanyakazi wote, wakiwemo wa kigeni na wafanyakazi wahamiaji na wale ambao wako katika sekta isiyo rasmi. Kiwango cha chini cha mshahara Zanzibar kilikuwa juu ya mstari wa umaskini.

Kiwango cha kawaida cha kazi kwa wiki ni masaa 45, pamoja na kiwango cha juu cha masaa tisa kwa siku au siku sita kwa wiki. Kazi yoyote inayozidi viwango hivyo inapaswa kufidiwa kwa malipo ya ovataimu ya mara moja na nusu ya mshahara wa kawaida wa mfanyakazi. Chini ya hali zilizo nyingi, ni haramu kuwapanga wanawake wajawazito na wanaonyonyesha watoto kufanya kazi kati ya saa 4 usiku na saa 12 asubuhi.

Sheria inaelezea kwamba wafanyakazi wenye ajira ya miezi 12 wanastahili siku 28 za likizo yenye malipo kwa mwaka, na inahitaji wafanyakazi wafidiwe sikukuu za kitaifa. Sheria inakataza ovataimu ya kupindukia au ya lazima, na inazuia

ovataimu hadi masaa 50 katika kipindi cha wiki nne, au kulingana na mikataba ya kazi iiyokubaliwa awali. Sheria inahitaji malipo sawa kwa kazi sawa.

Sheria kadhaa zinadhibiti viwango vya usalama na afya kazini (OSH). Kulingana na TUCTA, viwango vya OSH vinafaa kwa viwanda vikuu na utekelezaji wa viwango hivyo ulikuwa ukiboreka, lakini changamoto zilibakia katika sekta binafsi. Mnamo Machi Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilitoa ripoti ya ufuatiliaji kuhusu ukaguzi wa utendaji wa mwaka 2013 juu ya usimamizi wa afya na usalama nchini. Ukaguzi huo uligundua kwamba mapendekezo mengi yalikuwa yametekelezwa kikamilifu.

Viwango vya OSH, hata hivyo, havikutekelezwa kwa ufanisi katika uchumi usio rasmi. Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini haikuajiri wakaguzi wa kutosha. Kisheria wafanyakazi wanaweza kujiondoa wenyewe kutokana na hali ambayo inahatarisha afya au usalama wao bila ya kuhatarisha ajira zao, lakini mamlaka hazikuimarisha kwa ufanishi ulinzi huo.

Wafanyakazi wanaweza kumshtaki mwajiri kama hali zao za kazi hazifuati viwango vya mazingira na afya vya Wizara ya Kazi. Kwa ujumla migogoro ilitatuliwa kupitia kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Hakukuwa na tofauti kwa wafanyakazi wowote wa kigeni au wahamiaji.

Wafanyakazi wengi hawakuwa na mikataba ya ajira na walikosa ulinzi wa kisheria. LHRC iliripoti kwamba wafanyakazi wengi hawakuwa na mikataba ya maandishi, na wale waliokuwa nayo mara nyingi hawakupatiwa nakala za mikataba yao. Zaidi ya hayo waajiri mara nyingi waliweka nakala za mikataba zilizotofautiana na maelezo ambayo wafanyakazi walipewa. Makampuni mara nyingi yalitumia mikataba ya muda mfupi wa miezi sita au chini ili kuepuka kuajiri wafanyakazi wenye ulinzi wa kazi.

Serikali haikutekeleza viwango vya kazi kwa ufanisi, hasa katika sekta isiyo rasmi, ambako wafanyakazi walio wengi wameajiriwa. Adhabu hazikutosha kuzuia ukiukwaji. Idadi ya wakaguzi haikutoshi kuzuia ukiukwaji.

Katika viwanda hatari kama vile vya ujenzi, wafanyakazi mara kwa mara walifanya kazi bila ya vifaa vya kinga kama vile helmeti, kofia ngumu na glovu, au lijamu. Kulingana na Utafiti wa Taarifa za Ajali ya mwaka 2008 (wa hivi karibuni unaopatikana), sekta zenye viwango vilivyo vya juu vya ajali zenye mauti ni ujenzi na majengo, usafiri, na uchimbaji madini na uvujanji wa mawe. Wafanyakazi wa majumbani waliripotiwa kuwa waathiriwa wa dhuluma wa mara kwa mara.